https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness




https://www.path-2-happiness.com/sw

# MITUME NA MANABII

https://www.path-2-happiness.com/sw

# Yaliyomo

**MITUME NA MANABII**

JE, WATU WANA HAJA NA MITUME?

UKWELI WA UTUME NA UJUMBE WAKE

DALILI ZA UTUME

MISINGI YA DA'WAH YA MITUME

HISTORIA YA ULUL-'AZM

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



# MITUME NA MANABII

## JE, WATU WANA HAJA NA MITUME?

Mwenyezi Mungu ameumba viumbe wake katika umbile (fitra) sahihi, na akawawekea akili ili waweze kupambanua baina ya haki kwenye batili, na kwa sababu akili za wanadamu zina mapungufu na udhaifu, matamanio na maslahi, bali na migongano ndani yake.

Katika hali hiyo wanachokiona baadhi ya watu kuwa ni kizuri na wema wengine wanaweza kukiona kuwa kibovu, bali hata mtu mmoja anaweza kubadilika rai yake kwa kubadilika kwa zama na mahali, pamoja na kuwa akili hizo haziwezi kudiriki kilichojificha katika hali halisi katika elimu mbali mbali, kadhalika hawezi kudiriki muradi wa Muumba, maamrisho yake na makatazo yake, mbali na kuwa mwanadamu hawezi kupokea kutoka kwa Allah moja kwa moja, Allah amesema: {Na haikuwa kwa mwanaadamu kwamba Mwenyezi Mungu amsemeze ila kwa Wahyi (Ufunuo), au kwa nyuma ya pazia, au kumtuma Mjumbe. Naye humfunulia ayatakayo kwa idhini yake. Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye hikima.} [42:51]

Hivyo basi Allah akachagua viumbe vyake bora zaidi miongoni mwa Mitume na Manabii ili wawe mabalozi wazuri baina yake Yeye Allah na waja wake, Allah amesema: {Mwenyezi Mungu huteuwa Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.} [22:75],

Ili wawaongoze watu katika kumuabudu Yeye, na wawaondoshe kwenye dhuluma za kiza na kuwapeleka katika uongofu wa Nuru, ili watu wasiwe na

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



hoja kwa Allah baada ya kupelekewa Mitume –Allah amesema: {Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:165].

Hivyo basi suala la kutuma Mitume kwa watu likawa ni jambo kubwa la neema kwa watu kutoka kwa Allah; ili awafundishe kinachowafaa na kinachowatakasa, Allah amesema: {Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi.} [3:164].

Kwa hakika neema kubwa kutoka kwa Allah ni kuwatumia watu Mitume, na Mtume huyo kuwa {miongoni mwao},

### Kuwa mtu Usio na Makuu

"Hata katika kilele cha utukufu wake Muhammad alidumu katika hali yake, alikuwa akichukia anapoingia sehemu yenye kundi la watu wakamsimamia au kupitiliza katika kumkaribisha."

**Washington Irving**
Mwanadiplomasia na mwanafasihi wa Kimarekani



neema hii inaonekena dhahiri na wazi kuwa Mtume huyu ametumwa na Allah akizungumza na watu kwa maneno matukufu ya Allah Ta'ala, akizungumza na watu kuhusu dhati ya Allah na sifa zake na kuwaeleza ukweli wa Uungu na sifa zake, mbali mbali, kisha akawalingania katika yale yatakayofanya maisha yao yawe mazuri, na awaongoze katika kitakachofaa mioyo yao na hali zao mbali mbali, na kuwalingania na kuwaita katika Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, huu ni ukarimu mkubwa wa neema hii, fadhila hii na utoaji huu? Bali huwatoharisha na huwanyanyua na huwasafisha, husafisha mioyo yao na fikra zao na hisia zao, na husafisha nyumba zao, heshima zao na Swala zao, na hutoharisha maisha yao, jamii zao, na mifumo yao, na huwasafisha wao na uchafu wa ushirikina, upagani na upotofu na masimulizi potofu, na yale ambayo yanapatikana katika maisha haya katika minasaba mbali mbali na desturi mbovu zisizofaa kwa mwanadamu na maana ya utu wake.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Vivyo hivyo kuwasafisha na uchafu wa maisha ya kijaahiliya, na uchafu ulioenea katika hisia za watu, katika itikadi zao na ufahamu wao wa mambo mbali mbali.

Ujahilia ni Ujahilia, na kila ujahilia una uchafu wake, haijalishi huo ujahilia uko wapi kulingana na zama na mahali, pale ambapo nyoyo za watu zikaepuka na akida ya kiungu inayohukumu muono wao katika sharia ambayo inatokana na akida hii-ambayo ndio itakayohukumu maisha yao basi bila shaka kitakachokuwepo hapa kitakuwa ni Ujahilia katika sura zake mbali mbali, na hapana budi kumuokoa mwanadamu na Ujahilia huu iwe ujahilia huu ni wa zama hizi au wa zama za kale, Ujahiia ndio huo huo, Ujahilia uwe ni ule wa zamani au wa leo hii-sifa zote za Jaahiliya zitapatikana kwenye sifa zile za Ujahilia wa zamani katika upande wa tabia (Akhlaq) na wa kijamii, na utaweka malengo ya maisha ya mwanadamu na hali kadhalika upeo wake (mwisho wake)! Pamoja na kuwa ufunguzi wa elimu za maendeleo na makubwa ya kielimu na viwanda na teknolojia: {…ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.} [62:2]

Upotevu katika mtazamo na itikadi, na upotevu katika malengo ya maisha ni upotevu katika desturi na mifumo, na (tabia), ni upotofu katika nidhamu (mfumo) ni upotevu katika jamii na tabia.



https://www.path-2-happiness.com/sw

### Wanadamu ni Wanyama wanapokataa Dini

Katika takwimu katika moja ya vyuo vikuu nchini Marekani ambavyo yaliandikwa katika kitabu (Amerika ina swali au haiswali) ya David Parton kuwa:

-Asilimia themanini 80% ya wanawake Marekani hubakwa mara moja katika maisha yao!!


-Idadi ya wanawake wenye kubakwa kila siku ni zaidi ya wasichana 19000. Matokeo ya hilo ni kuwa kiasi cha asilimia thelathini 30% ya wasichana huko Marekani ima hupata mimba au hutoa mimba au kujifungua katika umri wa miaka kumi na nne.

-Asilimia sitini na moja (61%) za ya hali ya kubakwa ilikuwa kwa wasichana chini ya miaka kumi na nane.

-Asilimia 29% ya ubakaji ilikuwa kwa watoto chini ya miaka kumi na moja

**David Parton**

Mwandishi wa Kimarekani



## UKWELI WA UTUME NA UJUMBE WAKE

Miongoni mwa hekima ya Allah Ta'ala ni kuwa kila Mtume ni miongoni mwa jinsi ya watu anaowatumia Mtume, Allah amesema: {Nasi hatukuwatuma kabla yako ila watu wanaume tulio wapa Wahyi (Ufunuo)….} [16:43]

Na azungumze kwa lugha ya watu wake ili wafahamu maneno yake, na maana yake, Allah amesema: {Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa kaumu yake ili apate kuwabainishia. Basi Mwenyezi Mungu humuacha akapotea amtakaye, na akamwongoa amtakaye. Naye ni Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima.} [14:4]

Mitume wote husafika kwa utimilifu wa akili na usalama wa fikra zao, na ukweli na uaminifu wa kupokea amana za watu na kuhifadhi, na kuepushwa na dhambi ambayo huharibu mwenendo wa mwanadamu, na viwili wili

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



vyao kuepushwa na vinavyochukiza na macho kutazama, Allah ametakasa nafsi zao na tabia zao, wao ni watu wakamilifu zaidi kwa tabia, na wenye nafsi zilizotakaswa zaidi na mikono yenye ukarimu. Allah Ta'ala amekusanya kwao tabia njema kama alivyokusanya kwao uvumilivu, elimu, usamehevu, ukarimu, ushujaa na uadilifu; kiasi cha kupambanuka katika tabia hizi baina ya watu wao, Mitume ni watu bora zaidi katika viumbe vyake, Mwenyezi Mungu amewachagua kubeba ujumbe na kufikisha amana, Allah amesema: {…Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi anaweka ujumbe wake….} [6:124]

Na akasema: {Hakika Mwenyezi Mungu alimteuwa Adam na Nuhu na ukoo wa Ibrahim na ukoo wa Imran juu ya walimwengu wote.} [3:33]

Na akasema kuhusu Issa ('Alayhi salaam): {Na pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo kwake. Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa walio karibishwa (kwa Mwenyezi Mungu). Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utuuzima wake, na atakuwa katika watu wema.} [3:45-46],

Na Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alijulikana kwa watu wake kama "Mkweli mwaminifu." Kabla ya kuteremshwa kwa utume, na Mola wake akamsifu kwa: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4].

Hawa Mitume na Manabii pamoja na sifa alizowasifu nazo Allah Ta'ala miongoni mwa sifa tukufu, ila wao ni watu yanawafika yanayowafika watu wote, wao wanasikia njaa, wanaugua, wanalala, wanakula, wanaoana na wanakufa, Allah amesema: {Na hakika Sisi tulikwisha watuma Mitume kabla yako, na tukajaalia wawe na wake na dhuriya….} [13:38],

Na akasema Mtukuka: {Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa.}[39:30]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na akasema kuhusu Mtume wake Muhammad: {…Na ukaficha nafsini mwako aliyo taka Mwenyezi Mungu kuyafichua…} [33:37].

Na katika hali hiyo huenda wakateswa, au wakauwawa, au wakafukuzwa kwenye miji yao, Allah amesema: {Na walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.} [8:30]

Lakini mwisho wake wao kupata ushindi duniani na akhera.



## DALILI ZA UTUME

Mitume na Manabii ambao Allah amewatuma kwa waja wake ni lazima Allah awasimamishie hoja na dalili zinazobainisha ukweli wa Da'wah yao, yenye kuhakikisha kuwa wao ni Mitume wa Allah ili hoja isimame kwa watu, na kusiwe na udhuru kwa kutowasadikisha na kuwatii, Allah amesema: {Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi} [57:25].

Miongoni mwa dalili muhimu sana katika hizo ni:

Allah anawapa Mitume na Manabii kwa aya mbali mbali na miujiza, ambayo Allah huipitisha katika mikono ya Mitume na Manabii wake katika mambo ambayo yanavunja mazoea ya kawaida ya kimaumbile ambazo mwanadamu hawezi kufanya, mfano wa hayo ni alama ya Musa ('Alahyi Salaam) pale fimbo yake ilipogeuka kuwa nyoka, Allah amesema: {Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa? Akasema: Hii ni fimbo yangu; naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu. Tena inanifaa kwa matumizi mengine. Akasema: Itupe, ewe Musa! Akaitupa. Mara ikawa nyoka anaye kwenda mbio. Akasema: Ikamate, wala usiogope! Tutairudisha hali yake ya kwanza. Na uambatishe mkono wako kwenye ubavu. Utatoka mweupe pasipo kuwa na madhara yoyote. Hiyo ni ishara nyengine. Ili tukuonyeshe baadhi ya ishara zetu kubwa. } [20:17-23]

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



https://www.path-2-happiness.com/sw


Na alama ya Issa ('Alahyi Salaam) alipokuwa akiponya mbalanga na ukoma kwa idhini ya Allah, katika ndimi ya Mariam Allah amesema akimbashiria Issa: {Maryamu akasema: Mola wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali hajanigusa mwanaadamu? Mwenyezi Mungu akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huumba apendacho. Anapo hukumu jambo, huliambia: Kuwa! Likawa. Na atamfunza kuandika na Hikima na Taurati na Injili. Na ni Mtume kwa Wana wa Israili kuwaambia: Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakwambieni mnacho kila na mnacho weka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika haya ipo Ishara kwenu ikiwi nyinyi ni wenye kuamini. Na ninasadikisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlio harimishiwa, na nimekujieni na Ishara kutokana na Mola Mlezi wenu. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nit'iini mimi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi muabudni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka. } [3:47-51]

Na alama kubwa kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ambayo ni Qur-aan, pamoja na yeye kutokusoma

kilichoandikwa, Allah amesema: {Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao. Na hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'ani kwa kila mfano. Lakini watu wengi wanakataa isipo kuwa kukanusha tu.} [17:88 -89].

Na aya nyinginezo kuhusu Mitume na Manabii.

Na kwa kufuatilia na kusoma aya na miujiza ambayo Allah Ta'ala amewapa Mitume na Manabii wake tunaona zinaingia katika mambo matatu: Elimu, uwezo na kujitosha (utajiri) hivyo basi kutoa habari kuhusu mambo ya ghaibu yaliyopita na yajayo; kama vile Issa ('Alahyi Salaam) alivyowaambia watu wake chakula watakachokula na watakachohifadhi katika majumba yao-na Mtume wetu Muhammad kuelezea kuhusu Umma zilizotangulia na kuwajulisha kuhusu mitihani mbali mbali na dalili za Kiama ambazo zitakuja baadae–yote hayo yanatokana na elimu, na kubadilika fimbo kuwa nyoka, na kuponya mbalanga na ukoma, na kufufua watu na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuepushwa na madhambi, na katika mlango wa kudura, na kumlinda kwa aliyetaka kumdhuru, Allah amesema: {Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri.} [5:67], Mambo haya matatu: elimu, uwezo, na kujitosha (utajiri), ambayo miujiza inarejea haifai





### Muujiza wa Milele

"Kwa hakika miujiza ya Manabii waliomtangulia Muhammad katika uhalisia ilikuwa ni miujiza ya wakati maalumu. Ambapo tunaweza kuiita Qur-aan muujiza wa milele: kwani taathira yake ni yenye kudumu na kuendelea. Ni rahisi kwa muumini katika zama na mahali popote kuona muujiza huu kwa kusoma tu katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Katika muujiza huu tunapata sababu ya kuenea kwa kasi kwa Uislamu. Kuenea ambako sababu yake wazungu hawaifahamu; kwa sababu hawajui Qur-aan, au ni kwa sababu hawaifahamu ila kupitia kwenye tafsiri ambazo hazinufaishi kwenye maisha achilia mbali kuwa si sahihi."

**Etienne Denier**

Mchoraji na Mwanafikra wa Ufaransa

https://www.path-2-happiness.com/sw



https://www.path-2-happiness.com/sw

kuwa katika sura ya ukamilifu ila kwa Allah Ta'ala.

1. Bishara ya Manabii waliotangulia kwa Manabii wanaofuatia:


Katika dalili za ukweli wa utume ni manabii waliotangulia kutabiri kuja kwa manabii wanaofuatia, Allah amechukua ahadi na mkataba (Mithaqi) ya kila Mtume ya kuwa lau akimtuma Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalam) katika maisha yake watamuamini, Allah Ta'ala amesema: {Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.} [3:81].

2. MTAZAMO KATIKA HALI ZA MANABII

Manabii na Mitume walikuwa wakiishi na kuchanganyika na watu wao na kuamiliana pamoja nao; na hivyo kuwa rahisi kwa watu kujua nyendo zao, na kujua ukweli wao, hivyo basi pale walipomtuhumu Maryam na mwanae Mtume wa Allah Issa ('Alahyi Salaam) Allah alidhihirisha ukweli wao, Allah amesema: {Akenda naye (mwanawe) kwa jamaa zake amembeba. Wakasema: Ewe Maryamu! Hakika umeleta kitu cha ajabu! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba. Akawaashiria (mtoto). Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi? (Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii. Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai, Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu. } [19:27-33].



https://www.path-2-happiness.com/sw



## Ukristo wa Kweli

"Kwa hakika dini ya Ukristo ambayo Muhammad alitaka kuirejesha kwenye asili yake safi kama ambavyo Masihi mwenyewe alivyoibashiri inakwenda kinyume na mafundisho ya siri ambayo ameyatangazwa Paulo na makosa makubwa aliyoyaingiza yaliwagawa sana wakristo.
Matarajio ya Muhammad na hamu yake ni kuwa baraka ya dini ya Ibrahim isiwe kwa watu wake peke yake tu, bali ienee kwa watu wote. Hivyo basi dini yake ya kati kwa kati ikawaongoza na kuwastaarabisha watu milioni nyingi na kama sio dini hii wengi wangeendelea kuzama katika ushenzi na ndio maana wakaupata udugu huu kupitia dini hii ya Kiislamu."

**Laitner**
Mustashrik kwa Kiingereza

Hivyo ndivyo Issa alivyozungumza utotoni. Makureishi walikuwa wakimuita Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kabla ya kutimilizwa kwake kuwa ni 'Mkweli Mwaminifu; na hiyo ni kutokana na ukweli wake na uaminifu wake, Qur-aan imeelekeza hilo; ili kutoa dalili ya ukweli wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa sababu maisha yake binafsi yalikuwa ni dalili kubwa, Allah amesema, {Sema: Mwenyezi Mungu angeli taka nisingeli kusomeeni, wala nisingeli kujuvyeni. Kwani nalikwisha kaa nanyi umri mzima kabla yake! Basi, je! Hamzingatii?} [10:16].

3. MUONO WA DA'WAH YA MTUME

Miongoni mwa dalili za utume na kuafikiana Da'wah ya Mtume katika misingi yake pamoja na misingi ya Da'wah ya Mitume na Manabii wote, hivyo Mtume analingania kwenye Tawhid ya Allah Ta'ala: kwani hili ndilo lengo ambalo kwa ajili yake Mwenyezi Mungu ameumba na kutuma Mitume,



https://www.path-2-happiness.com/sw

Allah amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.} [21:25]

Na akasema: {Na waulize Mitume wetu tulio watuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah'mani?} [43:45]


Akasema: {Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha.} [16:36]

Na katika yote haya ndio iliyokuwa da'wah ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) Mtume alikuwa ni sawa na wanadamu wengine ila alifadhilishwa na kukirimiwa na Wahyi, Allah amesema: {Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi.} [18:110],

Hivyo basi hawezi kulingania ufalme au uraisi, Allah Ta'ala amesema: {Sema: Mimi sikwambiini kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu. Wala sijui mambo yaliyo fichikana. Wala sikwambiini kuwa mimi ni Malaika. Mimi sifuati ila yanayo funuliwa kwangu. Sema: Je, wanakuwa sawa, kipofu na mwenye kuona. Basi hamfikiri?} [6:50]

**Ushahidi wa Kweli**

"Hakuna siku Muhammad ambavyo alijinasibisha na Uungu au nguvu yoyote ya kustaajabisha. Kinyume chake alikuwa na pupa juu ya maandiko, kuwa yeye alikuwa ni Mtume tu wa Mwenyezi Mungu amemtengeneza kufikishia watu WAHYI.



**Rom Landau**

Mkosoaji wa Uingereza

https://www.path-2-happiness.com/sw

Wala hawawaulizi watu ujira wa Da'wah yake atoayo Allah amezungumza akiwaelezea Mitume yake Nuuh, Huud Swalah, Luut na Shu'ayb kuwa waliwaambia kaumu yake: {Na sikutakini juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote. } [26:109] {Kadhalika katika aya zifuatazo vile vile} [26:127, 145, 164 na 180]

Na Muhammad akawaambia watu wake: {Sema (Ewe Mtume): Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.} [38:86]

### Kujivua kwa ajili ya Mungu

"Pamoja na kuwa Muhammad alikuwa ni bwana katika Bara Arabu: Hakufikiria lakabu, wala hakushughulika kuyakuza, bali aliendelea kuwa katika hali yake akitosheka kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuwa yeye ni Mtumishi wa Waislamu: Husafisha nyumba yake mwenyewe na hushona viatu vyake kwa mkono wake, alikuwa ni mtu mwema na mkarimu kama vile mapito ya upepo, Hakusudiwi na fukara yoyote wala mtu dhalili ila atampa alichonacho, na alichonacho kilikuwa ni kidogo kisicho mtosha yeye mwenyewe.".

**Lady Evelin Cobbold**

Mwanamama wa Kiingereza

4. NUSURA YA ALLAH NA KUUNGWA KWAO MKONO:

Katika dalili za ukweli wa manabii na waliotumwa vile vile ni Allah kuwanusuru na kuwahifadhi; itaingiaje akilini mtu adai utume au unabii nae ni muongo katika Da'wah yake, halafu baada ya hapo Allah atawalie kumnusuru,

https://www.path-2-happiness.com/sw


kumuhifadhi, kumuunga mkono na kueneza Da'wah yake, bali hilo halitoshi wala hamteremshii adhabu yake!! Allah amesema: {Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali, na hichi haramu - mkimzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa.} [16:116] Na akasema Mtukuka, {Na lau kama angeli tuzulia baadhi ya maneno tu, Bila ya shaka tungeli mshika kwa mkono wa kulia, Kisha kwa hakika tungeli mkata mshipa mkubwa wa moyo!} [69:44 -46].

## Mimi ni mwanadamu kama nyinyi

"Ama kwa hakika Muhammad  haiba halisi ya historia, bila yeye Uislamu usingeweza kupanuka na kuongezeka… wala hakusita hata mara moja kusema kuwa yeye ni binadamu kama wengine mwisho wake ni mauti, na kuwa yeye anatafuta msamaha na maghufira (kufutiwa dhambi) kwa Mwenyezi Mungu. Hata kabla ya kifo chake alitaka kusafisha dhamira yake kwa kila kosa dogo alilolifanya. Akasimama mara moja akihutubia: "Enyi Waislamu, kama nitakuwa nimempiga yeyote huu hapa mgongo wangu mtu alipize kisasi chake, au nimemnyang'anya mali yake basi mali yangu ni miliki yake."

**Henry Serouya**

Mustashrik wa Kifaransa





https://www.path-2-happiness.com/sw



# MISINGI YA DA'WAH YA MITUME

Da'wah ya Mitume yote imewafikiana katika misingi maalumu; msingi wa da'wah ya Mitume ni mmoja, Allah Ta'ala amesema: {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo…} [42:13];

Na ndio maana dini ya Mitume yote ikawa ni moja, Allah amesema, {Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayo yatenda. Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi nicheni Mimi.} [23:51-52],

Pamoja na sheria zake kutofautiana, Allah amesema, {Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake} [5:48],

Na lau sheria zingetokea kuwa kinyume na misingi ile basi ingetokea katika hekima, maslahi na huruma, bali ni muhali kuja kinyume na aliyokuja nayo, Allah amesema: {Na lau kuwa Haki ingeli fuata matamanio yao, basi zingeli haribika mbingu na ardhi na waliomo ndani…} [23:71],



Na katika kadhia mbalimbali ambazo Mitume wameafikiana na katika ujumbe wake mbali mbali ni:- -Kumuamini Allah, Malaika wake, kitabu chake, Mitume wake, Siku ya Mwisho, na Qadar kheri na shari yake, Allah Mtukuka amesema: {Mtume ameamini yaliyo teremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumet'ii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni kwako.} [2:285].

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Amri ya kumuabudu Allah Peke Yake bila ya kumshirikisha yeye na chochote na kumtakasa na kuwa na mke na mtoto, mfano na kuabudu masanamu, Allah Mtukuka amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} [21:25]

Vivyo hivyo amri ya kufuata njia yake, na kutofuata njia tofauti, na kutekeleza ahadi, na kupima sawa sawa kwa kilo na mizani na wema kwa wazazi wawili na uadilifu baina ya watu na ukweli katika kauli na amali, na kuharamisha maovu yaliyodhihiri na yaliyojificha na uovu na kudhulumu, na kuharamisha kuua watoto, na kuua nafsi pasina haki, na kukataza riba na kula mali ya mayatima, na kukataza ubadhirifu na kiburi na kula mali za watu kwa batili. Imani ya siku ya mwisho; kila mtu ana elimu ya yakini kuwa kuna siku ambayo atakufa, lakini nini baada ya kifo chake? Je, ni mwenye furaha au huzuni? Na kila Mitume na Manabii walifikisha na kuwaambia watu wao kuwa watafufuliwa na kulipwa malipo yao, ikiwa kheri basi atalipwa kheri na ikiwa shari atalipwa shari, na jambo hili la kufufuliwa na kuhesabiwa-akili zilizo salimika zinalikubali, na kuungwa mkono na sheria za Mwenyezi Mungu, kwa hakika Muumba mwenye uwezo, mwenye elimu, mwenye hekima ametakasika kuumba viumbe hivi hivi kwa mchezo na bila ya lengo na kuwaacha hivi hivi tu. Allah amesema, {Na hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya walio kufuru. Ole wao walio kufuru kwa Moto utao wapata.} [38:27]

Bali amewaumba viumbe wake kwa hekima kubwa, na kwa lengo tukufu zaidi, Allah amesema, {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi} [51:56]

Si laiki kwa (Mwenyezi) Mungu huyu mwingi wa hekima kuwafanya sawa wenye kutii na waasi na wale wenye kumfuata na kumuasi Allah amesema, {Je! Tuwafanye walio amini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au tuwafanye wachamngu kama waovu?} [38:28];

Hivyo basi ilikuwa ni ukamilifu wa hekima yake na ukubwa wa kudura yake Yeye Allah kuwalipa waja wake kwa matendo yao Siku ya Kiama; hivyo basi mwema atapewa thawabu na atamuadhibu mkosaji, Allah amesema:

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

{…ili awalipe kwa uadilifu wale walio amini na wakatenda mema. Na walio kufuru, wao watapata vinywaji vinavyo chemka, na adhabu chungu kwa sababu ya walivyo kuwa wakikufuru.} [10:4];

Hivyo basi ni wepesi kiasi gani kuhuisha watu kwa ajili ya kuhesabiwa kwao baada ya mauti, si ndio yeye (Subhaanahu wa Ta'ala) aliyeumba Mbingu na Ardhi?! Na Yeye Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameumba viumbe bila mfano uliotangulia, Je, hawezi kurudi kuumba mara nyingine?! Allah amesema: {Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliye ziumba mbingu na ardhi, na hakuchoka kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.} [46:33]

Na akasema Mtukuka: {Kwani aliye ziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi.} [36:81]

Kwa hiyo mwenye kuweza kuanzisha kitu mwanzoni ana uwezo wa kukirejesha tena, Allah amesema: {Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake. Naye ndiye mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [30:27];

## Misingi Misafi

"Uislamu sio dini mpya kutoka kwa Muhammad, lakini ilipoanza kusambaa ardhini baada ya kupita miaka mia sita ya kupaishwa mbinguni kwa masihi. WAHYI wa pili ulianza kushuka, ulikuwa ni ule ule unaounga dini za mbinguni na kuzirejesha kwenye asili yake safi. Mitume wote waliotumwa na Mwenyezi Mungu walikuwa Waislamu na ujumbe wao ulikuwa ni mmoja daima."

**Deborah Potter**

Mwanahabari wa Kimarekani



https://www.path-2-happiness.com/sw

Bali ilishatokea kufufuliwa kwa wafu katika maisha haya ya duniani kwa idhini ya Mwenyezi Mungu mbele ya Nabii Ibrahim ('Alahyi Salaam), {Na alipo sema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe vipi unavyo fufua wafu. Mwenyezi Mungu akasema: Kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue. Akamwambia: Twaa ndege wane na uwazoeshe kwako, kisha uweke juu ya kila kilima sehemu, kisha wete, watakujia mbio. Na ujue kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, na Mwenye hikima.} [2:260]

Na ilitokea hivyo hivyo kwa Issa ('Alahyi Salaam) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Allah amesema, {Na pale Mwenyezi Mungu atapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipo kutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani. Na nilivyo kufunza kuandika na hikima na Taurati na Injili. Na ulipo tengeneza udongo sura ya ndege, kwa idhini yangu, kisha ukapuliza ikawa ndege kwa idhini yangu; na ulipo waponesha vipofu na wakoma kwa idhini yangu; na ulipo wafufua wafu kwa idhini yangu; na nilipo kukinga na Wana wa Israili ulipo wajia na hoja zilizo wazi, na wakasema walio kufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu!} [5:110]

**Tawhidi halisi**

"Mtume wa Waarabu Muhammad kwa sauti kutoka kwa Mola wake, amewaita waabudu masanamu, wafuasi wa Ukristo na Uyahudi yaliyopotoka kwenye dini safi ya Tawhidi, na hivyo kuridhia kuingia katika mgogoro mkubwa pamoja na makundi mengine ya watu ambayo yanampeleka mtu katika kumshirikisha Muumba na miungu mingine."



**Laura VecciaVaglieri**

Mustashrik wa Kitaliano

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



# HISTORIA YA ULUL-'AZM

Watu walikuwa katika uongofu na wakatofautiana, Allah akatuma Mitume, ili awafundishe watu na awaonye:

{Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri} [62:2]

Lakini watu wakagawanyika kulingana na da'wah ya Mitume katika makundi mawili; kundi lililokubali (lililosadikisha) Mitume na kuamini, na kundi lililokadhibisha Mitume na kuwakana na kile walichokuja nacho, waliwakadhibisha kwa ujeuri; {Watu wote wa likuwa ni umma mmoja. Mwenyezi Mungu akapeleka Manabii wabashiri na waonyaji. Na pamoja nao akateremsha Kitabu kwa Haki, ili kihukumu baina ya watu katika yale walio khitalifiana. Na wala hawakukhitalifiana ila wale walio pewa Kitabu hicho baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya uhasidi baina yao. Ndipo Mwenyezi Mungu kwa idhini yake akawaongoa walio amini kwendea haki katika mambo waliyo khitalifiana. Na Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye kwenye Njia Iliyo Nyooka.} [2:213]

Na walikadhibisha kwa kiburi na kufuata matamanio yao, {…Basi kila walipo kufikieni Mitume kwa yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mlijivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawauwa.} [2:87].

Allah Ta'ala ameamrisha Mitume wote waaminiwe, {Semeni nyinyi: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyo teremshiwa sisi, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zake, na waliyo pewa Musa na Isa, na pia waliyo pewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatutafautishi baina ya yeyote katika hao, na sisi tumesilimu kwake.} [2:136],

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



Na akawaahidi watakaoamini Mitume kupata furaha, na uokozi hapa duniani na akhera, na akawakamia watakaokufuru na kuupa mgongo kupata khasara na tabu hapa duniani kabla ya kesho akhera, Allah amesema,

{Na atakaye fanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.} [5:56]

Na akasema vile vile:

{Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua! Wale walio amini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.} [13:28-29]

Na akasema kwa wale waliokufuru Mitume:

{Msiwadhanie walio kufuru kwamba watashinda katika nchi. Na makaazi yao ni Motoni, na hakika ni maovu kweli marejeo yao} [24:57].

Kila Mtume alikuwa na adui zake, Allah amesema:

{Na kadhaalika tumemfanyia kila Nabii maadui mashet'ani wa kiwatu, na kijini, wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba-pamba, kwa udanganyifu. Na angeli penda Mola wako Mlezi wasingeli fanya hayo. Basi waache na wanayo yazua.} [6:112],

Kisha waliokadhibisha waliwafanyia jeuri Mitume na kuwafanyia uadui, na wakawafanyia istihzai na kuwadharau, Allah amesema:{Na hakuwafikia Mtume ila walimkejeli.} [15:11]

Na akasema Mtukuka:{Na hawajii Nabii yeyote ila walikuwa wakimkejeli.} [43:7]

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na akasema Mtukuka: {Na hakika Mitume walio kabla yako walifanyiwa kejeli, lakini walio wafanyia kejeli wakaja kuzungukwa na yale yale waliyo kuwa wao wanayafanyia kejeli.} [6:10]

Na hali kadhalika wakawatishia kuwafukuza na kuwatoa katika miji yao, au warudi katika dini zao, Allah amesema, {Na walio kufuru wakawaambia Mitume wao: Tutakutoeni katika nchi yetu, au mrudi katika mila yetu. Basi Mola wao Mlezi aliwaletea wahyi: Hakika tutawaangamiza walio dhulumu!} [14:13],

Vitisho hivyo vikafikia kiasi cha kuwauwa, {…Na kila taifa lilikuwa na hamu juu ya Mtume wao wamkamate….} [40:5],

Yaani kumuuwa, kiasi cha miongoni mwao kuuwa Mitume wao, {…Basi kila walipo kufikieni Mitume kwa yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mlijivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawauwa} [2:87],

Mwenyezi Mungu baada ya hapo akawaangamiza waliokadhibisha na akadhihirisha dini ya Mitume, kama alivyosema Allah Ta'ala: {Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.} [58:21]

Na akasema Mtukuka: {Na bila ya shaka neno letu lilikwisha tangulia kwa waja wetu walio tumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakao nusuriwa.} [37:171-172]

Na Allah aliokoa Mitume wake wote, kama Allah alivyosema: {Na tukawaokoa wale walio amini na walio kuwa wanamchamngu.} [27:53]

Na akasema vile vile: {Na tukawaokoa walio amini na wakawa wanamcha-mngu.} [41:18]

Na kila Mtume aliyekwenda kwa watu wake na kulazimiana na



**Marcel Boisard**
Mwanafikra wa Kifaransa

**Kutoka katika taa moja.**

"Hakukuwepo ndani ya ujumbe wa Muhammad kubatilisha yaliyoteremshwa kabla yake; bali ni kusadikisha upungufu uliovikumba vitabu vya mbinguni kama vile; kubadilisha na kuvunja sheria, na ukalazimishwa kusafisha mafundisho ya Mitume waliyotangulia katika kila kosa. Hivyo kupanuka ndani yake na kuenea kwake: ili iwafae wanadamu wote katika kila zama na mahali."

https://www.path-2-happiness.com/sw

yanayonasibiana nao kutengeneza maisha yao na kuwatakasa; Basi ambaye atakadhibisha Mtume mmoja, ni kama vile amewakadhibisha Mitume wote, yule ambae hamuamini Issa ('Alahyi Salaam) basi kihakika hatokuwa amemwamini Musa ('Alahyi Salaam), na Muhammad akafuta ujumbe wa Issa ('Alahyi Salaam) Allah amesema:

{Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda. Basi hukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao ukaacha Haki iliyo kujia….} [5:48]

Kwa hivyo basi ambaye hatomuamini Muhammad kihakika hatakuwa amemuamini Issa ('Alahyi Salaam). Na kuwa ni lazima kuwe Mtume wa mwisho kwa ajili ya watu wote na mahali pote, na sio kwa muda maalumu au fulani, vinginevyo Walimwengu wangepotea na kuangamia bila ya kuwepo msaada wa Wahyi kutoka kwa Muumba wa Ardhi na Mbingu. Hivyo basi Muhammad akawa ndiye Mtume wa mwisho Allah amesema,

{Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu} [33:40]



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



# NI IPI HISTORIA YA MANABII NA MITUME AMBAYO NDIO HISTORIA YA WANADAMU?

Tunaanzia pale Allah alipotaka kumuumba mwanadamu mpaka kumtoa Adam Peponi na kuteremka ardhini, {Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka
a uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa
tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi
ua. Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha
a Malaika, na akasema: Niambieni majina ya hivi ikiwa
Wakasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi
yo tufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye
Ewe Adam! Waambie majina yake. Basi alipo waambia
a: Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni
inayajua mnayo yadhihirisha na mliyo kuwa mnayaficha?
ulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam, wakamsujudia
isipo kuwa Iblis, alikataa na akajivuna na akawa katika
afiri. Na tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika
ani, na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini
karibie mti huu tu; mkawa katika wale walio dhulumu.
i Shet'ani aliwatelezesha hao wawili na akawatoa katika
o kuwamo, na tukasema: Shukeni, nanyi ni maadui nyinyi
nyinyi. Katika ardhi yatakuwa makaazi yenu na starehe kwa
a. Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola wake Mlezi,
lola wake Mlezi alimkubalia toba yake; hakika Yeye ndiye
Mwingi wa kukubali toba na Mwenye kurehemu. Tukasema: Shukeni nyote; na kama ukikufikieni uwongofu utokao kwangu, basi watakao fuata uwongofu wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Na wenye kukufuru na kuzikanusha ishara zetu, hao ndio watakao kuwa watu wa Motoni, humo watadumu.} [2:30-39].

**Hatutofautishi baina yao.**

"Qur-aan tukufu ni kitabu cha pekee ambacho kinakiri uwepo wa vitabu vingine kutoka mbinguni. Wakati ambapo tunaona vitabu vyote hivyo kila kimoja kinakataa vingine."

**Bashir Shaad**

Mhubiri wa India.



Kisha baada ya hapo watu wakaupa mgongo uongofu na haki, ndipo alipotuma Mitume wake, Mitume wakafuatana pamoja na sheria zao; {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo.} [42:13]



https://www.path-2-happiness.com/sw

Kisha wakafuatana Mitume wa Allah kutokea Idriss hadi Nuhu, Ibrahim, Ismail, Musa, Issa na Muhammad (Swalawatu Llahi Wasalamuhu alayhim jami'an). Allah ametutajia visa vyao na kutujulisha habari zao, hapa tutataja kidogo kuhusu visa vya baadhi yao; kwani visa vyao vimejaa mazingatio kwa wenye akili, Allah Ta'ala amesema: {Kwa hakika katika hadithi zao limo zingatio kwa wenye akili. Si maneno yaliyo zuliwa, bali ni ya kusadikisha yaliyo kabla yake, na ufafanuzi wa kila kitu, na ni uwongofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini} [12:111];



Miongoni mwa visa hivyo ni:-

## 1. NUUH ('Alayhi salaam)

Watu wake hapo kabla walikuwa ni waumini, wakimuabudu Allah peke yake, wakiamini Siku ya Mwisho, na wakifanya mambo mema, watu wale akafa, watu wakahuzunika kwa wema wao na tabia zao njema wakatengeneza picha zao (Wakawapa majina yafuatayo: Wadda, Yaaghutha,Yaa'uqa, Nasra, watu wakavutika na picha zile na…) wakafanya ndio alama za wale watu wema waliokufa miongoni mwao, watu wa mjini wakatukuza picha zile, wakikusudia kuwatukuza wafu wale muda ukapita wale watu wazima wakafa na kubaki watoto na kuwa wakubwa, wakawa wanaongezea namna mbali mbali za kutukuza, na kunyenyekea mbele zao, picha na sura

https://www.path-2-happiness.com/sw

zile zikawa na nafasi kubwa katika mioyo ya watu wale, ama kizazi cha pili kilichofuatia wakawa wamejiwekea sheria ya kuabudu sura zile na kusema kuwa ile ni miungu inabidi wayasujudie na kunyenyekea mbele yake; wakawa wanayaabudu, wengi wakapotea kwa kufanya hivyo.

Baada ya hapo Allah akawatumia watu wale Mtume Nuhu ('Alahyi Salaam); ili awaelekeze njia (iliyonyooka), na kuwakataza kuabudu masanamu, na kuwaelekeza kumuabudu Allah Ta'ala, Nuhu ('Alahyi Salaam) akaenda kwa kaumu yake… {…Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mungu asiye kuwa Yeye…} [23:23]

Wakamkadhibisha, na hawakumkubali, akawaonya na kuwatahadharisha adhabu ya Allah Ta'ala. Akasema: {Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Kubwa.} [26:135],

Wakasema: {Wale watukufu katika kaumu yake wakasema: Hakika sisi tunakuona wewe umo katika upotofu ulio dhaahiri.} [7:60],

Nuhu akawajibu: {Akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika upotofu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote. Nakufikishieni Ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na ninakunasihini; na ninayajua kwa Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi.} [7:61-62]

Watu wakashangazwa na maneno ya Nuhu, wakawa wanasema. Wewe ni mtu kama sisi, utakuwaje Mtume kutoka kwa Allah? Na ambao wamekufuata ni kundi la watu dhaifu na watu wa chini, kisha hamna ubora kutushinda sisi, si katika mali wala katika vyeo, na sisi tunadhania kuwa mnadanganya katika madai yenu haya, baadhi ya kaumu wakawaambia wengine: {…Huyu si chochote ila ni mtu tu kama nyinyi. Anataka kujipa ubora juu yenu. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu amependa basi yakini angeli teremsha Malaika. Hatukusikia haya kwa baba zetu wa zamani. Huyu si lolote ila ni mtu mwenye wazimu…} [23:24-25]

Baadhi yao wakahamasisha wengine kuabudu masanamu yao: {Na wakasema: Msiwaache miungu yenu, wala msimwache Wadda wala Suwaa' wala Yaghutha, wala Yau'qa, wala Nasra.} [71:23].

Nuhu ('Alayhi salaam) akawaambia: {Je, mnastaajabu kukujieni mawaidha yanayotoka kwa Mola Mlezi wenu kwa njia ya mtu aliye ni mmoja katika nyinyi, ili akuonyeni…} [7:63]

Na baada ya hapo Nuhu akawachukulia kwa upole na ulaini, lakini watu waliendelea na inadi yao, na akawalingania wakati wote mpaka akasema: {Akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimewaita watu wangu usiku na mchana, Lakini wito wangu haukuwazidisha ila kukimbia. Na hakika mimi kila nilipo waita ili upate kuwaghufiria, walijiziba masikio yao kwa vidole vyao, na wakajigubika nguo zao, na wakakamia, na wakatakabari vikubwa mno! } [71:5-7]

Akawalingania katika kila njia iliyowezekana: {Tena niliwaita kwa uwazi, Kisha nikawatangazia kwa kelele, tena nikasema nao kwa siri.} [71: 9-10],

Wengine wakajiundia nyudhuru duni kwa kusema: {Wakasema: Je! Tukuamini wewe, hali wanao kufuata ni watu wa chini?} [26:111]

Nuhu akawajibu kwa upole na ulaini na kuwakumbusha: {Akasema: Nayajuaje waliyo kuwa wakiyafanya?} [26:112]

Kisha akawaambia: {Hisabu yao haiko ila kwa Mola wao Mlezi, laiti mngeli tambua!} [26:113]

Hoja ikakamilika, udhuru ukakatika, na da'wah ikaendelea takriban karne Kisha Nuhu akasema tena: {Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini.} [26:114],

Na, {na mimi sitawafukuza walio amini} [11:29].



Vipi nitawafukuza watu ambao wameniamini, wamenihami na wamenisaidia kutangaza da'wah?! Kisha akawaambia: {Na enyi watu wangu! Ni nani atakaye nisaidia kwa Mwenyezi Mungu nikiwafukuza hawa? Basi je, hamfikiri?} [11:30], {Mimi si cho chote ila ni Mwonyaji wa dhaahiri shaahiri.} [26:115].Ninawaonya watu sawa kwa sawa, bila kutofautisha kati ya mtukufu na mnyonge, tajiri na fukara, mkubwa na mdogo na mweupe na mweusi…, watu walipokatikiwa na hoja na kushindwa kujibu dalili za Nuhu, wakawa wanamtisha kumpiga mawe: {Wakasema: Ikiwa huachi, ewe Nuhu, bila ya shaka utapigwa mawe.} [26:116].



**Ujumbe wa Mwisho.**

"Muhammad ni Mtume aliyeleta Uislamu; na hivyo kuwa kipengele cha mwisho katika mnyororo wa Mitume ambao wamebeba ujumbe mkubwa."

**Pro. Rolf Baron**

Profesa wa Vyuo Vikuu vya Austria

Nuhu alipokuwa na yakini kuwa hawakubali maelezo yoyote (mantiki), wala hawaongoki, alinyenyekea kwa Allah amuokoe dhidi ya watu wale wenye inadi, {Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha.} [26:117]

{Basi hukumu baina yangu na wao kwa hukumu yako, na uniokoe mimi na walio pamoja nami, Waumini.} [26:118]

Pamoja na kuwa Nuhu alikuwa akihofisha kaumu yake na adhabu ya Allah, pindi watakapong'ang'ania ukafiri, baadhi yao walimjibu kwa kejeli: {…Basi tuletee hayo unayo tuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.} [11:32],

Nuhu akawajibu: "Jambo hili halipo katika mikono yangu": {Akasema: Mwenyezi Mungu atakuleteeni akipenda…} [11:33], {Wala nasaha yangu haikufaini kitu nikitaka kukunasihini…} [11:34].

Allah akamteremshia Wahyi: {…Hataamini yeyote katika watu wako ila wale walio kwisha amini. Basi usisikitike kwa waliyo kuwa wakiyatenda.} [11:36],

kumi, Nuhu alikata tamaa, akamuomba Mola wake, kwa kusema: {Na Nuh'u akasema: Mola wangu Mlezi! Usimwache juu ya ardhi mkaazi wake yeyote katika makafiri! Hakika ukiwaacha watawapoteza waja wako, wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.} [71:26-27].

Allah akamteremshia Wahyi wa kutengeneza Meli (Safina): {Tukampa wahyi: Unda jahazi mbele ya macho yetu na uwongozi wetu!...} [23:27]

Akaanza kutengeneza: {Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipita wakuu wa kaumu yake wakimkejeli….} [11:38]

Nuhu akawa anawajibu kwa adabu na upole: {…Yeye akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli na sisi tunakukejelini kama mnavyo tukejeli.} [11:38]

Kisha akiwaonya kwa adhabu ya Allah: {Nanyi mtakuja jua ni nani itakaye mfikia adhabu ya kumhizi, na itakaye mteremkia adhabu ya kudumu.} [11:39]

Na akafanya kazi kwa bidii, hadi alikamilisha kutengeneza Safina.

Kisha Allah akamuamrisha Nuhu kubeba katika safina ile wale walioamini pamoja nae, na kila chenye roho jozi mbili: {Hata ilipo kuja amri yetu, na tanuri ikafoka maji, tulisema: Pakia humo wawili wawili, dume na jike, kutoka kila aina, na ahali zako, isipo kuwa wale ambao imekwisha wapitia hukumu; na watu walio amini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.} [11:40]

Akawabeba wote walioamini pamoja nae jozi mbili mbili, {Na akasema: Pandeni humo kwa Bismillahi, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.} [11:41].

### Kiburi na uharibifu wa Historia.

"Katika karne ya kati Wakristo katika maandishi yao walianza kugawa watu kwa misingi ya kikabila na kitaifa kama ilivyotajwa katika agano la kale (Mwanzo) na kuongeza ugawaji wa tabaka jipya: Ikawa ni itikadi iliyoenea kuwa watu wa dini na makasisi wanatokana na kizazi cha Shemu. Wapiganaji wanatokana na kizazi cha Yafith. Mafukara wanatokana na kizazi cha Hamu watoto wa Nuhu ('Alayhi Salaam). Ilifikia kuwa katika mwaka 1964 kumpeleka Senata wa Marekani Robert Byrd kutoka mji wa Virginia ya Magharibi kutumia kisa cha Nuhu kama sababu ya kubaki sera ya ubaguzi katika Marekani.



Nuhu alipopanda na walioamini kwenye Safina pamoja nae, na akachukuwa wanyama, kila mmoja katika mahali pake, mbingu ikaanza kunyesha mvua kubwa, chemchem za ardhi zikaanza kububuja maji mengi: {Basi tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayo miminika. Na tukazipasua ardhi kwa chemchem, yakakutana maji kwa jambo lilio kadiriwa. Na tukamchukua kwenye safina ya mbao na kamba .Ikawa inakwenda kwa nadhari yetu, kuwa ni malipo kwa alivyo kuwa amekanushwa.} [54:11-14]

Nuhu akamuona mwanae ambae hakuamini pamoja nae akiwa anataka kukimbia ili asizame akamuita: {…Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi, wala usiwe pamoja na makafiri} [11:42]

Lakini mtoto alikataa imani, na akakataa nasaha za baba yake, alimjibu Nuhu kwa kusema: {Akasema: Nitakimbilia mlimani unilinde na maji….} [11:43]

Nuhu akamuonea huruma mtoto wake huku akisema: {(Nuhu) akasema: Leo hapana wa kulindwa na amri ya Mwenyezi Mungu ila aliye mrehemu mwenyewe...} [11:43],

Hapo hapo: {…Na wimbi likawatenganisha, akawa katika walio zama} [11:43]

Nuhu akamsikitikia mwanae, na kunyenyekea kwa Allah amuokoe mwanae. Allah alimuahidi kuwaokoa watu wake, Nuhu ('Alayhi salaam) akasema: {…Ee Mola Mlezi wangu! Hakika mwanangu ni katika ahali zangu, na hakika ahadi yako ni haki. Na Wewe ni Mwenye haki kuliko mahakimu wote.} [11:45].

Allah ambae alimuahidi kuwaokoa watu wake (familia yake) waliokuwa wema, alisema: {Akasema: Ewe Nuhu! Huyu si katika ahali zako. Mwendo wake si mwema….} [11:46],

Katika dini hakuna kuwepo mtu wa kati, huyo si katika watu wako, haitamnufaisha kuwa ni mwanao madamu hakumuamini Allah wala kumpwekesha.

Baada ya maji kufurika kila sehemu, na kila kafiri kuangamia: {Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako…} [11:44]

Na maji yalioyotoka chini ya ardhi kusita. Allah aliteremshaWahyi, {…Na Ewe mbingu! Jizuie...} [11:44]

na simama kunyesha mvua; mvua ikasimama: {…Basi maji yakadidimia chini…} [11:44]

Hilo ni jabali ambalo safina ilitia nanga juu yake, na Wahyi ukateremka kwa Nuhu ('Alayhi salaam): {…Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe…} [11:48]

Nuhu akateremka kutoka katika Safina, na wakataremka waumini waliokuwa pamoja nae, wakajenga mji, na kupanda miti na wakawaacha wanyama waliokuwa nao, na ardhi ikaanza kuimarishwa na watu kuzaana na kuenea.

**Mitume kudharauliwa.**

Nuhu akaanza kuwa mkulima, akapanda mizabibu; akanywa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake. Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje. Shemu na Yafethi wakatwaa vazi, wakalitanda mabegani mwao wote wawili, wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao; na nyuso zao zilielekea nyuma, wala hawakuuona uchi wa baba yao. Nuhu akalevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea. Akasema, Na alaaniwe Kanaani; Atakuwa mtumwa kabisakwa ndugu zake." (Mwanzo: 9:20-25) na hivyo akawabariki Shemu na Yafethi.
Katika tafsiri ya andiko hili Talmud Baabli imetaja. Kitabu Sanhadrin uk. 70 kuwa Kanaani au Hamu aligombana na Nuhu na kumfanyia maovu!! Kamwe haiwezekani kwa Nabii Mtukufu kufanya hivyo.



## 2. IBRAHIM ('Alayhi salaam)

Ibrahim ('Alahyi Salaam) Mtume wa Tawhidi, hilo linadhihiri katika Historia yake; hivyo ndio maana Allah akamsifu kwa kusema: {Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.} [16:120];

Ibrahim aliishi pamoja na kaumu ya washirikina, bali baba yake alikuwa mmoja wa wanaoabudu masanamu na mmoja miongoni mwa wanaoyatengeneza na kuyaabudu, Ibrahim akaanza kujadiliana na baba yake pamoja na kaumu yake: {Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake, Azar: Unayafanya masanamu kuwa ni miungu? Hakika mimi nakuona wewe na watu wako mmo katika opotofu ulio wazi.} [6:74]

Na akapinga yaliyokuwa kwa kaumu yake kwa hoja madhubuti ushirikina wao na akawa anaangalia katika alama na dalili za kuwepo kwake Allah Ta'ala: {Na ulipo muingilia usiku akiona nyota, akasema: Huyu ni Mola Mlezi wangu. Ilipo tua akasema: Siwapendi wanao tua.} [6:76];

Yaani: kuzama kwa nyota: {akasema: Siwapendi wanao tua. Alipo uona mwezi unachomoza…} [6:76-77],

Yaani: Kuchomoza kutoka kwenye upeo wa macho, na akaona baadhi ya watu wakiyaabudu: {…alisema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu…} [6:77].

Akapinga matendo yao, huku akistaajabia ibada zao!! Aliitumia fursa hiyo: {…Ulipotua…} [6:77];

Yaani kupotea chini ya upeo wa macho, alielekea kwa watu wake na kuwaambia: {…akasema: Kama Mola Mlezi wangu hakuniongoa, nitakuwa katika kaumu walio potea. …Na alipo liona jua linachomoza} [6:77-78],



https://www.path-2-happiness.com/sw

Na akawaona watu wakinyenyekea mbele yake: {…akasema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu. Huyu mkubwa kuliko wote….} [6:78]

Akapinga matendo yao!! Akashangazwa ni kwa nini wamefanya jua kuwa Mungu wao?! {…Lilipo tua…} [6:78],

Na kupotea machoni, aliwaelekea watu wale ambao walikuwa wakiiabudia, akawaambia: {…alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayo fanyia ushirikina. … Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa aliye ziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa washirikina.} [6:78-79].

Na alikuwa akimpa sana mawaidha baba yake na kumkataza ushirikina kwa utulivu, adabu na mantiki: {Sema: Nani anaye kulindeni usiku na mchana na Arrahmani Mwingi wa Rehema? Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao Mlezi. Au wao wanao miungu watao weza kuwakinga nasi? Hao hawawezi kujinusuru nafsi zao, wala hawatalindwa nasi! Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka umri ukawa mrefu kwao. Je, hawaoni ya kwamba Sisi tunaifikia ardhi tukiipunguza ncha zake? Basi je! Hao ni wenye kushinda? Sema: Mimi nakuonyeni kwa Wahyi. Na viziwi hawasikii wito wanapo onywa.} [21:42-45].



https://www.path-2-happiness.com/sw

Kwa bahati mbaya jibu la baba yake lilikuwa kali: {(Baba) akasema: Unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? Kama huachi, basi lazima nitakupiga mawe. Na niondokelee mbali kwa muda!} [19:46].

Jibu la Ibrahim lilikuwa la adabu ya hali ya juu, huruma na upole: {(Ibrahim) akasema: Salamun a'laika! Amani iwe juu yako! Mimi nitakuombea msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ananihurumia sana. Nami najitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Na ninamwomba Mola wangu Mlezi; asaa nisiwe mwenye kukosa bahati kwa kumwomba Mola wangu Mlezi.} [19:47-48]

Ibrahim aliendelea kuwalingania watu wake na baba yake kwa Allah na tawhidi yake na kuacha ushirikina, lakini watu wake hawakumuitikia Ibrahim na wakaendeea na ushirikina: {Na watu wake wakamhoji. Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ameniongoa? Wala siogopi hao mnao washirikisha naye, ila Mola wangu Mlezi akipenda kitu. Mola wangu Mlezi amekusanya ilimu ya kila kitu. Basi je, hamkumbuki? Na vipi nivikhofu hivyo mnavyo vishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu…} [6:80-81],

Na kwa mara nyingine akawaambia: {Alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini?} [26:70]

Wakamjibu: {Wakasema: Tunaabudu masanamu, daima tunayanyenyekea} [26:71], {Akasema: Je! Yanakusikieni mnapo yaita? Au yanakufaeni, au yanakudhuruni?}[26:72-73],

Likawa jibu la kipumbavu ambalo halitumii akili wala mantiki, kwa kuiga tu: {Wakasema: Bali tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo hivyo.}[26:74]

Akawajibu kwa kutumia tawhidi halisi kwa hoja na akili na busara: {Je! Mmewaona hawa mnao waabudu- Nyinyi na baba zenu wa zamani? Kwani hakika hao ni adui zangu, isipo kuwa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ambaye ndiye aliye niumba, na Yeye ndiye ananiongoa, Na ambaye ndiye ananilisha na kuninywesha. Na ninapo ugua ni Yeye ndiye anaye niponesha. Na ambaye atanifisha, na kisha atanihuisha. Na ambaye ndiye ninaye mtumai kunisamehe makosa yangu Siku ya Malipo. Mola wangu Mlezi! Nitunukie hukumu na uniunganishe na watendao mema. Na unijaalie nitajwe kwa wema na watu watakao kuja baadaye. Na unijaalie katika warithi wa Bustani za neema. Na umsamehe baba yangu, kwani hakika alikuwa miongoni mwa wapotovu.}[26:75-86].



Ilipofika sikukuu ya kaumu ile, mfalme pamoja na watu wake walikwenda uwanjani jangwani; ili watekeleze na kusherehekea sikukuu huko, Ibrahim hakutoka pamoja nao; walipondoka: "Nao wakamwacha, wakampa kisogo. Basi akaiendea miungu yao kwa siri, akaiambia: Mbona hamli? Mna nini hata hamsemi? Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa kulia. " [37:90-93],

Waliporudi wakakuta miungu yao imevunjwa, watakuwaje ni Miungu ambayo haiwezi kujitetea! Walikuja upesi: "Wakasema: Nani aliye ifanyia haya miungu yetu? Hakika huyu ni katika walio dhulumu. Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahim. Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia! Wakasema: Je! Wewe umeifanyia haya miungu yetu, ewe Ibrahim? " [21:59-62],

Akawajibu kwa hoja kubwa: {Akasema: Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao. Basi waulizeni ikiwa wanaweza kutamka.} [21:63]

Wakawa wadogo mbele ya hoja ile: {Basi wakajirudi nafsi zao, wakasema: Hakika nyinyi mlikuwa madhaalimu! Kisha wakarejea kwenye ule ule upotovu wao wakasema: Wewe unajua kwamba hawa hawesemi.} [21:64-65]

Akawajibu kwa hoja kubwa yenye nguvu: {Akasema: Basi nyinyi mnawaabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu wasio kufaini kitu wala kukudhuruni? Aibu yenu nyinyi na hivyo mnavyo viabudu badala ya Mwenyezi Mungu! Basi nyinyi hamtii akilini?} [21:66-67]

https://www.path-2-happiness.com/sw



Wakataka kulipa kisasi baada ya kukosa hoja, mantiki na dalili: {Wakasema: Mchomeni moto, na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo!} [21:68]

Allah akamuokoa: {Sisi tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim! Wao walimkusudia maovu, lakini Sisi tukawafanya wao ndio walio khasiri.} [21:69-70].

Baada ya Allah kumuokoa, akarudi na kujadiliana na mfalme wao: {Hukumwona yule aliye hojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa ufalme? Ibrahim alipo sema: Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na kufisha….} [2:258],

Mbele ya hoja hii yenye nguvu iliyo wazi imekuja kuwa jibu la (mfalme) mpumbavu: {…Yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha…} [2:258],

Ibrahim hakubishana nae kwenye kuropoka huku, na kutoka katika mjadala huu kuwa anaweza kumuua mtu na kumuacha mtu: {… Ibrahim akasema: Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi. Akafedheheka yule aliye kufuru; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.} [2:258]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Udhaifu wa hoja, dalili na mantiki yao ukadhihirika; na baada ya mjadala Ibrahim akataka aone waziwazi namna ambayo Mola wake atahuisha: {Na alipo sema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe vipi unavyo fufua wafu. Mwenyezi Mungu akasema: Kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue. Akamwambia: Twaa ndege wane na uwazoeshe kwako, kisha uweke juu ya kila kilima sehemu, kisha wete, watakujia mbio. Na ujue kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, na Mwenye hikima.} [2:260].

Allah akamuamrisha Ibrahim pamoja na mwanae Ismail kusafisha nyumba ya Allah ya Makka kutokana na ushirikina na masanamu: {…Na tuliagana na Ibrahim na Ismail: Itakaseni Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kut'ufu na wanao jitenga huko kwa ibada, na wanao inama na kusujudu. Na alipo sema Ibrahim: Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea. Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipo inyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi. Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe umma ulio silimu kwako. Na utuonyeshe njia za ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.} [2:125-128].




**Msikiti wa Ibrahim Al-Khalil katika msikiti wa Al-Ibrahimy katika mji wa Al-Khahil huko Palestina.**

# 3. MUSA ('Alahyi Salaam)

Bani Israil walikuwa wakisomeshana wenyewe kuhusiana na Mtume Ibrahim ('Alahyi Salaam) kuwa katika kizazi chake atatoka kijana ambae mfalme wa Misri ataangamia kwa mikono yake, utabiri huu ulikuwa ni maarufu kwa Bani Israil. Habari zile zikafika kwa Firauni na maamiri wake walimueleza habari hiyo, hivyo kuamuru kuuwawa kwa wavulana wa Bani Israil kwa kutahadhari na kuwepo kwa kijana huyo. Zama hizo Bani Israil walikuwa wanaishi kwa kuonewa shida na dhuluma kubwa kutoka kwa Firauni: {Hakika Firauni alitakabari katika nchi, na akawagawa wananchi makundi mbali mbali. Akalidhoofisha taifa moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na akiwaacha watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa katika mafisadi.} [28:4]

Allah akataka kuwaneemesha waliodhoofishwa miongoni mwa Bani Israil: {Na tukataka kuwafadhili walio dhoofishwa katika nchi hiyo na kuwafanya wawe waongozi na kuwafanya ni warithi. Na kuwapa nguvu katika nchi, na kutokana na wao kuwaonyesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyo kuwa wakiyaogopa.} [28:5-6].

Pamoja na Firauni kujihadhari na kukwepa kutopatikana Musa, kiasi cha kuwafanya askari wake wakiwazungukia wenye mimba na wakijua tarehe za kuzaa kwao, hivyo basi alikuwa hazai mwanamke yoyote mtoto wa kiume isipokuwa watamchinja wachinjaji hao muda ule ule, Lakini Allah alitaka kumuoneshe Firauni, Hamana na majeshi yake walichokua wakitahadhari. Pindi mama yake Musa alipozaa: {Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapo mkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa Mitume.} [28:7]

Hivyo akawa na khofu juu yake, akamuweka katika sanduku la mbao na kumtupa mtoni:{Basi wakamwokota watu wa Firauni, aje kuwa adui kwao na huzuni. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa.} [28:8].

Mapenzi ya Musa yakaingizwa moyoni mwa mke wa Firauni: {Na mkewe Firauni alisema: Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako. Msimuuwe! Huenda akatufaa, au tumpange kuwa mwenetu. Wala wao hawakutambua.} [28:9]

Ama mama yake Musa: {Na moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu. Alikuwa karibu kumdhihirisha, ingeli kuwa hatukumtia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa Waumini. Naye akamwambia dada yake Musa: Mfuatie. Basi naye akawa anamuangalia kwa mbali bila ya wao kujua.} [28:10-11]

{Na tukamjaalia awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo, mpaka dada yake akasema: Je! Nikuonyesheni watu wa nyumba watakao mlea kwa ajili yenu, nao pia watakuwa wema kwake? Basi tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, lakini wengi wao hawajui.} [28:12-13].



Musa akakulia katika nyumba ya dhalimu muovu Firauni: {Na Musa alipo fika utu-uzima baraabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyo walipa walio wema. Na akaingia mjini wakati wa kughafilika wenyeji wake, na akakuta humo watu wawili wanapigana - mmoja ni katika wenzake, na mwengine katika maadui zake. Yule mwenzake alimtaka msaada kumpiga adui yake. Musa akampiga ngumi, akamuuwa. Akasema: Hiki ni kitendo cha Shet'ani; hakika yeye ni adui, mpotezaji dhaahiri. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe. Akamsamehe; hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu. Akasema: Mola wangu Mlezi! Kwa ulivyo nineemesha, basi mimi sitakuwa kabisa msaidizi wa wakosefu.} [28:14-17].

Lakini baada ya kuua adui yake na adui wa Bani Israil: {Akapambazukiwa mjini asubuhi naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Mara yule yule aliye mtaka msaada jana akawa anampigia kelele amsaidie. Musa akamwambia: Hakika wewe ni mgomvi kweli kweli. Basi alipo taka kumshika kwa nguvu yule aliye adui wao wote wawili, akasema: Ewe Musa! Unataka kuniuwa kama ulivyo muuwa mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi, wala hutaki kuwa miongoni mwa wenye maslaha.. Na akaja mtu kutoka mwisho wa mji akipiga mbio, akasema: Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuuwa. Basi toka! Hakika mimi ni katika wanao kupa nasaha. Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhaalimu.} [28:18-21],

Aliondoka Misri na kuelekea Madyan: {Na alipo elekea upande wa Madyana alisema: Asaa Mola wangu Mlezi akaniongoa njia iliyo sawa. Na alipo yafikia maji ya Madyana alikuta umati wa watu wananywesha (wanyama wao), na akakuta karibu yao wanawake wawili wanawazuia wanyama wao. Akasema: Mna nini? Wakasema: Hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao wachunga. Na baba yetu ni mzee sana. Basi Musa akawanyweshea; kisha akarudi kivulini, na akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia.} [28:22-24].

Wale wasichana wawili wakamwambia baba yao –Nabii wa Allah Shu'ayb – alichokuwa nacho, Nabii wa Allah Shu'ayb ('Alahyi Salaam), akamtuma mmoja wa binti zake kwa Musa ('Alahyi Salaam): {Basi mmoja katika wale wanawake wawili akamjia, naye anaona haya. Akasema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea….} [28:25].




Musa akafika kwa Shu'ayb ('Alayhima salaam): {…Basi alipo mjia na akamsimulia visa vyake, alisema: Usiogope; umekwisha okoka kwenye watu madhaalimu.} [28:25],

Binti yake mmoja alipoona uaminifu wa Musa ('Alahyi Salaam): {Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.} [28:26]

Shu'ayb akamtaka Musa ('Alayhima salaam): {Akasema: Mimi nataka kukuoza mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane. Ukitimiza kumi, khiari yako; lakini mimi sitaki kukutaabisha. Inshallah utanikuta miongoni mwa watu wema. Musa akasema: Hayo yamekwisha kuwa baina yangu na wewe. Muda mmojapo nikiumaliza sitiwi ubayani. Na Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu ya haya tunayo yasema. } [28:27-28].

Musa alipomaliza muda wake alisafiri kwenda kwa watu wake: {Basi alipo timiza muda wake na akasafiri na ahali zake, aliona moto upande wa Mlima T'uri. Akawaambia ahali zake: Ngojeni! Mimi nimeona moto, labda nitakuleteeni kutoka huko khabari au kijinga cha moto ili mpate kuota moto.} [28:29],

Hapo ndipo Allah alipomteremshia Wahyi:



{Basi alipo ufikia aliitwa kutoka ng'ambo ya bonde la kuliani katika eneo lilio barikiwa kutoka kwenye mti: Ewe Musa! Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Na tupa chini fimbo yako. Basi alipo iona ikitikisika kama nyoka, akarudi nyuma wala hakutazama. (Akaambiwa): Ewe Musa! Njoo mbele wala usiogope. Hakika wewe ni miongoni mwa walio salimika. Ingiza mkono wako kwenye mfuko wako, utatoka mweupe pasipo na ubaya. Na jiambatishe mkono wako ukihisi khofu. Basi hizi ni dalili mbili zitokazo kwa Mola wako Mlezi kumpelekea Firauni na wakuu wa umma wake. Hakika hao walikuwa watu mafaasiki.} [28:30-32],

Lakini Musa alimuogopa Firauni kwa sababu alimuua adui yake hapo kabla, na kwa sababu ya fundo lililo kwenye ulimi wake: {Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nilimuuwa mtu katika wao, kwa hivyo naogopa wataniuwa. Na ndugu yangu Harun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume ende nami kunisaidia, ili anisadikishe. Hakika mimi nina khofu watanikadhibisha.} [28:33-34].



https://www.path-2-happiness.com/sw



Akamuomba Allah amfanye ndugu yake Harun, Waziri: {Na nipe waziri katika watu wangu, Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu. Na umshirikishe katika kazi yangu. Ili tukutakase sana. Na tukukumbuke sana. Hakika Wewe unatuona. Akasema: Hakika Umepewa maombi yako, ewe Musa! } [20:29-36].

Walipokwenda kwa Firauni na kumfikishia waliyotumwa katika kumlingania yeye kumuabudu Allah Ta'ala peke yake bila kumshirikisha na chochote na kufungua mateka wa Bani Israil na kuacha kuwakamata, kuwatenza nguvu na kuwanyanyasa na awaache wamuabudu Mola wao watakavyo, na wajishughulishe na kumpwekesha Allah peke yake na kunyenyekea kwake. Firauni akatakabari na kupetuka mipaka na akamuangalia Musa kwa jicho la dharau na kebehi akimwambia: {(Firauni) akasema: Sisi hatukukulea wewe utotoni, na ukakaa kwetu katika umri wako miaka mingi? Na ukatenda kitendo chako ulicho tenda, nawe ukawa miongoni mwa wasio na shukrani? } [26:18-19].

Musa akamjibu: {(Musa) akasema: Nilitenda hayo hapo nilipo kuwa miongoni mwa wale walio potea.} [26:20];

Yaani kabla sijateremshiwa Wahyi na kupewa utume: {Basi nikakukimbieni nilipo kuogopeni, tena Mola wangu Mlezi akanitunukia hukumu, na akanijaalia niwe miongoni mwa Mitume.} [26:21],

Kisha akasema akimjibu Firauni alivyojisifu kumlea na kumfanyia wema:

https://www.path-2-happiness.com/sw



{Na hiyo ndiyo neema ya kunisumbulia, na wewe umewatia utumwani Wana wa Israili?} [26:22];

Yaani neema hii uliyoitaja ya kwamba ulinifanyia mema na mimi ni mtu mmoja katika Bani Israil na kwa upande wa pili umewatumikisha watu hawa wa Bani Israil kwa ukamilifu na kuwafanya kuwa watumwa katika kukutumikia na kukuhudumia katika shughuli zako. Kisha Firauni akamuulizia Mola ambae Musa anamlingania: {Firauni akasema: Na nani huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote?} [26:23],

Likaja jibu linalo kinaisha: {Akasema: Ndiye Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi ni wenye yakini.} [26:24],

Firauni akaanza kebehi: {(Firauni) akawaambia walio mzunguka: Hamsikilizi?} [26:25],

Musa akaendelea na kulingania watu wote: {(Musa) akasema: Ndiye Mola wenu Mlezi, na Mola Mlezi wa baba zenu wa kwanza.} [26:26],

Firauni akazidisha uovu wake: {(Firauni) akasema: Hakika huyu Mtume wenu aliye tumwa kwenu ni mwendawazimu.} [26:27],

Hata hivyo, Mtume wa Allah Musa hakuacha kadhia yake: {(Musa) akasema: Ndiye Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi mnatia akilini.} [26:28],

Dikteta mkubwa mwenye kiburi na kujikweza Firauni aliyekosa hoja na akili na mantiki alianza vitisho: {(Firauni) akasema: Ukimfuata mungu mwengine asiye kuwa mimi, basi bila ya shaka nitakufunga gerezani.} [26:29],

Kama ambavyo kebehi na dharau za Firauni hazikumuondosha Musa katika da'wah yake, hata vitisho vya Firauni havikumfanya kuacha



da'wah yake; hivyo alimjibu: {Akasema: Je! Ijapo kuwa nitakuletea kitu cha kubainisha wazi? Akasema: Kilete basi, kama wewe ni katika wasemao kweli. Basi akaitupa fimbo yake, mara ikawa nyoka wa kuonekana dhaahiri. Na akautoa mkono wake, na mara ukawa mweupe kwa watazamao.} [26:30-33],

Firauni akaogopea watu wasije kumuamini (Musa), hivyo akawaambia watu wake: {(Firauni) akawaambia waheshimiwa walio mzunguka: Hakika huyu ni mchawi mtaalamu. Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake. Basi mna shauri gani? Wakasema: Mpe muda yeye na nduguye na uwatume mijini wapigao mbiu ya mgambo. Wakuletee kila mchawi bingwa mtaalamu. " [26:34-37]

Baada ya Firauni kuona hoja zote alifanya jeuri na kukana na kukataa: {Na hakika tulimwonyesha ishara zetu zote. Lakini alikadhibisha na akakataa. Akasema: Ewe Musa! Hivyo umetujia kututoa katika nchi yetu kwa uchawi wako? Basi sisi hakika tutakueletea uchawi kama huo. Basi weka miadi baina yetu na wewe, ambayo tusiivunje sisi wala wewe, mahali patapo kuwa sawa. Akasema: Miadi yenu ni siku ya Sikukuu; na watu wakusanywe kabla ya adhuhuri. Basi Firauni akarudi na akatengeneza hila yake, kisha akaja. } [20:56-60],

Musa akawaogopea kupata adhabu ya Allah: {Musa akamwambia: Ole wenu! Msimzulie Mwenyezi Mungu uwongo, asije akakufutilieni mbali kwa adhabu. Na mwenye kuzua lazima ashindwe!} [20:61];

Hivyo wakatofautiana, baadhi yao wakasema: haya si maneno ya mchawi: {Basi wakazozana kwa shauri yao wenyewe kwa wenyewe, na wakanong'ona kwa siri.} [20:62].

Lakini wao wakarejea, wengi wao wakasema: {Wakasema: Hakika hawa wawili ni wachawi, wanataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wao, na waondoe mila zenu zilizo bora kabisa. Kwa hivyo kusanyeni hila zenu zote, kisha mfike kwa kujipanga safu, na kwa yakini atafuzu kweli kweli leo atakaye



shinda.} [20:63-64] {Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio. } [20:66]

Musa akaogopea wale wachawi wasije wakawafitinisha: {Basi Musa akaingia khofu nafsi yake.} [20:67],

Allah akamteremshia Wahyi; Musa: {Tukasema: Usikhofu! Hakika wewe ndiye utakaye shinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyo viunda. Hakika walivyo unda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo.} [20:68-69], {Nasi tukamfunulia Musa kumwambia: Tupa fimbo yako. Mara ikavimeza vyote vile walivyo vibuni. Kweli ikathibiti na yakabat'ilika waliyo kuwa wakiyatenda.} [7:117-118],

Kwa ghafla (likatokea jambo lisilotarajiwa): {Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakageuka kuwa wadogo. Na wachawi wakapoomoka wakisujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa viumbe vyote, Mola Mlezi wa Musa na Haarun.} [7:119-122], {Basi wachawi wakaangushwa wanasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa Harun na Musa! } [20:70],

Vitisho vya Firauni vikaonekana kama upumbavu: {(Firauni) akasema: Oh! Mnamuamini kabla sijakupeni ruhusa? Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliye kufundisheni uchawi. Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende…. } [20:71],

Jibu lao halikutarajiwa kwa Firauni, na huu ni uthibitisho wa wazi jinsi Imani inavyomfanya aliyeamini: {Wakasema: Haidhuru, kwani sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi tunatumai Mola wetu Mlezi atatusamehe makosa yetu, kwa kuwa ndio wa kwanza wa kuamini.} [26:50-51].

Firauni akaendelea kuwaudhi waumini; Allah akamuadhibu pamoja na walio nae: {Na hakika tuliwaadhibu watu wa Firauni kwa miyaka (ya ukame) na kwa upungufu wa mazao, ili wapate kukumbuka. Likiwafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi. Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui. } [7:130-131],

Hawakuamini wala kutubia: {Na wakisema: Hata ukituletea Ishara yoyote

https://www.path-2-happiness.com/sw

kutuzuga hatuto kuamini. Basi tukawapelekea tufani, na nzige, na chawa, na vyura, na damu, kuwa ni Ishara mbali mbali. Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu.} [7:132-133],

Walipochoka:

{Na ilipo waangukia adhabu wakasema: Ewe Musa! Tuombee kwa Mola wako Mlezi kwa aliyo kuahidi. Ukituondolea adhabu hii hapana shaka tutakuamini, na tutawaachilia Wana wa Israili wende nawe. Lakini tukiwaondolea adhabu mpaka muda fulani wao waufikie, mara wakivunja ahadi yao.} [7:134-135],

Hawakutekeleza waliyoyaahidi, bali walitengua waliyoyasema:

{Basi tuliwapatiliza, tuka-wazamisha baharini kwa sababu walizikanusha Ishara zetu, na wakaghafilika nazo.} [7:136].

Watu wa Misri walipozama katika ukaidi, ukafiri na inadi yao na kumfuata mfalme wao, na kwenda kinyume na Nabii wao na Mtume wao Musa bin Imran (‘Alahyi Salaam), na baada ya Allah kuwasimamishia hoja kubwa na kuwaonesha miujiza, lakini pamoja na yote hayo hawakuacha wala hawakurudi nyuma, na hawakuamini isipokuwa wachache miongoni mwa kaumu ya Firauni.

Ama wachawi wote, na Bani Israil wote, Imami zao zilikuwa za kificho kwa kumuogopa Firauni na dhuluma zake, ujeuri na ubabe wa utawala wake. Mwenyezi Mungu alimteremshia wahyi Musa pamoja na nduguye Harun (‘Alahyi Salaam) wajiwekee majumba maalumu miongoni mwao tofauti na nyumba za watu wa Firauni; ili wawe katika matayarisho ya kuhama pindi watakapoamrishwa ili waweze kufahamiana nyumba zao, na ili wamuabudu Allah huko:

{Na tukampelekea Musa na ndugu yake wahyi huu: Watengenezeeni majumba watu wenu katika Misri na zifanyeni nyumba zenu ndio mwahali mwa ibada, na wabashirie Waumini.} [10:87].

https://www.path-2-happiness.com/sw



Kisha Allah akamteremshia Wahyi mja wake Musa:

{Na tulimuamrisha Musa kwa wahyi: Nenda na waja wangu wakati wa usiku. Kwa hakika mtafuatwa. } [26:52],

Jibu la Firauni likawa:

{Basi Firauni akawatuma mijini wapiga mbiu za mgambo. (Wakieneza): Hakika hawa ni kikundi kidogo. Nao wanatuudhi. Na sisi ni wengi, wenye kuchukua hadhari.} [26:53-56],

Na Allah akataka:

{Basi tukawatoa katika mabustani na chemchem, Na makhazina, na vyeo vya hishima, Kadhaalika; na tukawarithisha hayo Wana wa Israili.} [26:57-59]

Wakawafuata Bani Israil:

{Basi wakawafuata lilipo chomoza jua. } [26:60],

Walipofika kwa Bani Israil:

{Na yalipo onana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana! } [26:61],

Lakini jibu la Musa lilikuwa limejaa tumaini la Allah, kumjua na kumtegemea yeye Allah Ta'ala:

{(Musa) akasema: Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa!} [26:62],

Baada ya hapo hidaya ya Allah na rehma zake zikateremka:

{Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa.  Na tukawajongeza hapo wale wengine. Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote. Kisha tukawazamisha hao wengine. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara; lakini wengi wao si katika wenye kuamini. Na kwa hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.} [26:63-68].

Katika wakati huu mgumu wenye kutisha:

{Tukawavusha bahari Wana wa Israili, na Firauni na askari wake wakawafuatia kwa dhulma na uadui!...} [10:90],

Hapa ndipo Firauni alipoyakinisha mauti na kuangamia:

{…Hata Firauni alipo kuwa anataka kuzama akasema: Naamini kuwa hapana mungu ila yule waliye muamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa walio nyenyekea} [10:90],

Lakini alishachelewa; kwani mauti yalishamdiriki: {Ala! Sasa? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa mafisadi! } [10:91],

Mwenyezi Mungu akatimiza neema yake kwa Bani Israil kwa kumuangamiza adui yao na walipovuka bahari: {Na tukawavusha bahari Wana wa Israili, wakafika kwa watu wanao abudu masanamu yao. Wakasema: Ewe Musa! Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyo kuwa na miungu….} [7:138];

Yaani ombi la mjinga baada ya neema ya kuokolewa na Allah dhidi ya Firauni na majeshi yake: {…Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msio jua kitu. Hakika haya waliyo nayo watu hawa yatakuja angamia, na hayo waliyo kuwa wakiyafanya yamepotea bure.} [7:138-139],

Kisha Musa akaenda katika kiaga na Mola wake: {Tulimuahidi Musa masiku thalathini na tukayatimiza kwa kumi; ikatimia miadi ya Mola wake Mlezi masiku arubaini. Na Musa akamwambia nduguye Haarun: Shika mahala pangu kwa watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu. } [7:142],

Allah akazungumza na Musa na akamfanya mahsusi kwa maneno yake na ujumbe wake: {(Mwenyezi Mungu) akasema: Ewe Musa! Mimi nimekuteuwa wende kwa watu na Ujumbe wangu na maneno yangu. Basi chukua niliyo kupa na uwe katika wanao shukuru.} [7:144]

Na akamneemesha kwa mawaidha na Taurati ambayo ndani yake kuna hukumu za Allah: {Na tukamuandikia katika mbao kila kitu, mawaidha na maelezo ya mambo yote. (Tukamwambia): Basi yashike kwa nguvu na uwaamrishe watu wako wayashike kwa ubora wake. Nami nitakuonyesheni makaazi ya wapotofu.} [7:145],

Kiaga ilipotimia, na Mola wake akampa Musa Taurati, Musa alirudi kwa watu wake na akawakuta: {Na baada yake watu wa Musa walimfanya ndama kutokana na mapambo yao (kumuabudu), kiwiliwili tu kilicho kuwa na sauti. Hivyo, hawakuona kuwa hawasemezi wala hawaongoi njia? Wakamuabudu, na wakawa wenye kudhulumu. Na walipo juta na wakaona ya kwamba wamekwisha potea, walisema: Ikiwa Mola wetu Mlezi hakuturehemu na akatusamehe, bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa walio khasiri.} [7:148-149],




https://www.path-2-happiness.com/sw



Ikawa ni habari yenye kuumiza sana kwa Musa: {Na alipo rudi Musa kwa watu wake, naye amekasirika na kuhuzunika, alisema: Ni maovu yalioje mlio nifanyia nyuma yangu! Je, mmeitangulia amri ya Mola wenu Mlezi? Na akaziweka chini zile mbao, na akamkamata kichwa ndugu yake akimvutia kwake. (Haarun) akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Hakika hawa watu wamenidharau, na wakakaribia kuniuwa. Basi usiwafurahishe maadui juu yangu, wala usinifanye pamoja na watu madhaalimu. (Musa) akasema: Mola Mlezi wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na ututie katika rehema yako. Nawe ni Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.} [7:150-151],

Kisha akaongea na Saamiriy aliyetengeneza ndama yule, akasema: {(Musa) akasema: Ewe Msamaria! Unataka nini?} [20:95]

Akamjibu: {Akasema: Niliona wasiyo yaona wao, nikashika gao katika unyao wa Mtume. Kisha nikalitupa. Na hivi ndivyo ilivyo nielekeza nafsi yangu.} [20:96];



Jibu la Musa likawa jibu lenye nguvu lenye kukata hoja zote za kumshirikisha Allah: {(Musa) akasema: Basi ondoka! Na kwa yakini utakuwa katika maisha ukisema: Usiniguse. Na hakika una ahadi kwako isiyo vunjwa. Na mtazame huyo mungu wako uliye endelea kumuabudu - Sisi kwa hakika tutamchoma moto, kisha tutamtawanya baharini atawanyike. Hakika Mungu wenu ni Allah, Mwenyezi Mungu, tu. Hapana Mungu isipo kuwa Yeye. Ujuzi wake umeenea kila kitu. } [20:97-98],

Kisha Musa akaenda nao kuelekea ardhi tukufu, baada ya kuchukua mbao (za maandiko):{Na Musa ilipo mtulia ghadhabu aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake mna uwongofu na rehema kwa wanao mwogopa Mola wao Mlezi.} [7:154],

Baadhi ya Bani Israil walikuwa hawakubali yaliyomo katika Taurati; Allah akanyanyua Jabali juu yao: {Na pale tulipo unyanyua mlima juu yao ukawa kama kwamba ni kiwingu kilicho wafunika, na wakadhani kuwa utawaangukia, (tukawaambia): Kamateni kwa nguvu tuliyo kupeni, na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kumcha Mungu.} [7:171],



Hivyo wakachukua pamoja na kuwa kuna uongofu kwao na rehema kwa kuogopea jabali lisije kuwaangukia, wakaendelea kuwafanyia maudhi Bani Israil pamoja na Mtume wao Musa ('Alahyi Salaam). Basi mara moja wakauwa mtu, na mtu yule alikuwa ni Bani Israil tajiri, mtoto wa nduguye alimpitia usiku na akamchinja! Wakatofuatiana na kutuhumiana na kila mmoja akajitetea, wakamfuata Mtume wao Musa ('Alayhi salaam), na kumwambia kwa jeuri na adabu mbovu; ikiwa wewe Musa ni nabii basi muulize Mola wako! Allah akamuamrisha Musa: Ewe Musa waamrishe Bani Israil wachinje ng'ombe, kisha wachukue kiungo chake wampige nacho maiti; nami nitamuhuisha kwa idhini yangu; hivyo maiti Yule atazungumza na kumtaja aliyemuua, Allah amesema: {Na mlipo muuwa mtu, kisha mkakhitalifiana kwayo, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyatoa hayo mliyo kuwa mkiyaficha. Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (huyo ng'ombe). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.} [2:72-73],

https://www.path-2-happiness.com/sw



## As-Samiry – Mtengeneza Ndama wa Sanamu.

Haiwezekani Mtume wa Allah Harun kuwa ndie aliyetengeneza ndama na kulingania ushirikina: Mitume wote walikuwa ni walinganizi wa Tawhid. Atakayenukuu yasiyokuwa hayo amepotoka, mfano wa hayo yaliyokuja:
"Harun akawaambia: Zivunjeni pete za dhahabu zilizo katika masikio ya wake zenu, na wana wenu, na binti zenu, mkaniletee. Watu wote wakazivunja pete za dhahabu zilizo katika masikio yao, wakamletea Haruni. Akaipokea mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha; na wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyo kutoka katika nchi ya Misri." (Kutoka: 32/2-4). Agano la kale.

Musa akasema: Chinjeni ng'ombe, na wangemchukua ng'ombe yeyote ingetosha lakini kutokana na maudhi yao Allah akasema kwa ulimi wa Musa: {Na Musa alipo waambia watu wake: Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mchinje ng'ombe. Wakasema: Je! Unatufanyia mzaha? Akasema: Audhubil lahi! Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nisiwe miongoni mwa wajinga. } [2:67]

Watu wakajibu: {Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie ni ng'ombe gani?...} [2:68]

Walikazania nae Allah akawakazania: {…Akasema: Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu, wala si kinda….} [2:68]

Sio mkubwa mzee wala mdogo: {…Akasema: Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu, wala si kinda, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni mnavyo amrishwa.} [2:68]

Wakajifunga zaidi: {Wakasema: Tuombee kwa Mola wako atupambanulie nini rangi yake?...} [2:69],

Allah hakuwauliza rangi na hakuwawekea sharti maalumu: {…Akasema: Yeye anasema, kuwa ng'ombe huyo ni wa manjano, na rangi yake imekoza, huwapendeza wanao mtazama.} [2:69],

Wakakusanyika katika baraza maalum, kisha wakarudia maneno yao: {Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie ni yupi? Hakika tunaona ng'ombe wamefanana. Na kwa yakini, Inshaallah, Mwenyezi Mungu akipenda, tutaongoka. } [2:70],

Allah akawajibu: {Akasema: Yeye anasema: Kuwa huyo ni ng'ombe asiye tiwa kazini kulima ardhi wala kumwagia maji mimea, mzima, hana baka. Wakasema: Sasa umeleta haki. Basi wakamchinja, na walikaribia kuwa wasifanye hayo.} [2:71],

Wakatafuta katika miji na vijiji vya Bani Israil, kijiji hadi kijiji; wakampata ng'ombe huyu kwa tabu na taklifu kubwa na kwa thamani ghali mno; wakamchinja na hawakuwa wakitaka hilo, wakampiga maiti ambaye wametofautiana ni nani aliyemuua kwa sehemu ya kiungo cha ng'ombe yule; maiti Yule akaamka kwa kutetema na hasira; akaamka akiwa hai kutoka kaburini kwake kwa idhini ya Allah akiwa amesimama, Musa akamuuliza: Ni nani aliyekuuwa? Akasema: Huyu hapa: {Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (huyo ng'ombe). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.} [2:73].

Walipofika katika ardhi tukufu, waliwakuta watu wenye nguvu (majabari): {Na pale Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipo wateuwa Manabii kati yenu, na akakufanyeni watawala, na akakupeni ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu. Enyi watu wangu! Ingieni katika nchi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika. Wakasema: Ewe Musa! Huko wako watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia.} [5:20-22], {Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.} [5:24];

Allah akawakosoa kwa udhaifu wao, na akawaadhibu kwa upotofu na kuacha kwao jihadi na kwenda kinyume na Mtume wao, Musa akasema: {Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tutenge na hawa watu wapotovu. } [5:25],

Allah Mtukuka akamuitikia: {(Mwenyezi Mungu) akasema: Basi nchi hiyo wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi. Basi wewe usiwasikitikie watu wapotovu. } [5:26],

Wakawa wanatembea katika ardhi bila malengo usiku na mchana, asubuhi na jioni.





## 4. ISSA BIN MARYAM ('Alayhi salaam).

Baba yake Maryam ('Alahyi Salaam) alikuwa ni 'Imran, mja miongoni wa waja wa Bani Israil, alitokana na kizazi cha Dawud ('Alahyi Salaam), katika nyumba ya wacha-Mungu, mama yake Maryam alikuwa hashiki mimba, akatamani kupata mtoto; akaweka nadhiri kwa Allah kuwa akipata mimba atamtoa mwanae wakfu kuitumikia dini na msikiti mtukufu (yaani mpenzi katika nyumba tukufu):

{Alipo sema mke wa Imran: Mola wangu Mlezi! Nimekuwekea nadhiri kilichomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Hakika Wewe ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua. Basi alipo mzaa alisema: Mola wangu Mlezi! Nimemzaa mwanamke - na Mwenyezi Mungu anajua sana aliye mzaa - Na mwanamume si sawa na mwanamke. Na mimi nimemwita Maryamu. Nami namkinga kwako, yeye na uzao wake, uwalinde na Shet'ani aliye laaniwa.} [3:35-36];

Allah akamkubalia mama yake Maryam nadhiri yake:

{Tena Mola wake Mlezi akampokea kwa mapokeo mema na akamkuza makuzo mema…} [3:37]

Katika sura nzuri na mandhari ya furaha na njia ya waja wema wenye furaha; na hivyo basi Allah akasema: {…na akamfanya Zakariya awe mlezi wake…} [3:37]

Allah akamneemesha kwa mlezi wake ni nabii vile vile, inasemwa kuwa alikuwa ni mume wa mama yake mdogo au mume wa dada yake: {…Kila mara Zakariya alipo ingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimwambia: Ewe Maryamu! Unavipata wapi hivi? Naye akasema: Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.} [3:37]

Ukarimu na utawala wa Allah kwake yeye, hivyo Mola wake akamkirimu, kumchagua, kumtoharisha, kumkamilisha na kumuamrisha kumuabudu: {Na angalia pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuteuwa, na akakutakasa, na akakutukuza kuliko wanawake wote. Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao.} [3:42-43],

Kisha Allah alipotaka Maryam amzae Issa (‘Alahyi Salaam) alijitenga na watu wake: {Na mtaje Maryamu katika Kitabu, pale alipo jitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki; Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Roho wetu, akajifananisha kwake sawa na mtu.} [19:16-17]

Maryam akaogopa, akimdhania kuwa anataka kumfanyia uovu: {(Maryamu) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe, ukiwa ni mchamngu. (Malaika) akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi ili nikubashirie tunu ya mwana aliye takasika.} [19:18-19],

Maryam akashangaa: {Akasema: Nitampataje mwana hali mwanaadamu yeyote hajanigusa, wala mimi si kahaba?} [19:20].

Yule mjumbe akamwambia hii ni hukumu ya Allah, na Mwenyezi Mungu amekufanya kuwa aya (dalili) na jambo hilo ni jepesi kwake: {(Malaika) akasema: Ndio hivyo hivyo! Mola wako Mlezi amesema: Haya ni mepesi kwangu! Na ili tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu, na Rehema itokayo kwetu, na hilo ni jambo lilio kwisha hukumiwa.} [19:21],

Kwa hiyo katika ambayo Mwenyezi Mungu ameyataka ni ishara ya kuzaliwa kwa Issa (‘Alahyi Salaam) kutoka kwa mama aliyetoharika ambae hakuzini au kufanya maovu na bila ya kuwa na baba (hii ni rehema



kutoka kwa Allah na utekelezaji wa hukumu ya Allah Ta'ala. Hivyo kuzaliwa Issa ('Alahyi Salaam) kukawa ni muujiza, miongoni mwa miujiza na aya miongoni mwa aya zake, mfano wake katika hilo ni mfano wa kuumbwa Adam bila baba:

{Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; alimuumba kwa udongo kisha akamwambia: Kuwa! Basi akawa. Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanao fanya shaka.} [3:59-60].

Aliposhika mimba alijiweka mbali na watu wake: {Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa mbali. } [19:22]

Uzazi ukamjia: {Kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende; akasema: Laiti ningeli kufa kabla ya haya, na nikawa niliye sahaulika kabisa!} [19:23],


Na hapa ndipo kulipotokea muujiza mwingine kwa Nabii wa Allah (Issa ('Alahyi Salaam): {Pakatangazwa kutoka chini yake: Usihuzunike! Hakika Mola wako Mlezi amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji! Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako. Na pindi ukimwona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu.} [19:24-26],

Na aliporejea kwa watu wake, kukutana nao kulikuwa kubaya kwa Maryam mwenye kutoharika mwenye

**Manabii ni watu bora zaidi.**

"Baadhi ya yaliyopotoshwa juu ya Mitume ya Allah na manabii inataja kuwa walilewa, au kuangukia katika uzinifu, au kuamrisha kuwa watu ni yote hayo ni upotofu mbayo haifai na hailingani na watu wenye tabia za juu mbali ya kuwa wao ni watu waliokuwa bora zaidi…. Wao ni Manabii wa Allah, katika hayo ni yale yaliyokuja – katika Taurati kuhusu Dawudi ('Alayhi Salaam) (Samweli (2) 11/2-26) na kutoka kwa Yoshua bin Nuun (mwana wa Nuni) ('Alayhi Salaam) (Yoshua 6/24) na kutoka kwa Musa ('Alayhi Salaam) (Hesabu:31/14-18) Musa ('Alayhi Salaam), na mengine mengi yasiyokuwa hayo hayafai Mtume wa Allah."





kujihifadhi: {Akenda naye (mwanawe) kwa jamaa zake amembeba. Wakasema: Ewe Maryamu! Hakika umeleta kitu cha ajabu! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba. } [19:27-28],

Nae hakuwajibu, bali: {Akawaashiria (mtoto)….} [19:29],

Wakachukizwa wakasema: {… Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi?} [19:29], {(Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii. Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai, Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu. Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa, na siku nitakayo kufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai.} [19:30-33],

Lakini kundi moja la Mayahudi halikuamini, wakamtuhumu Al-Twahira kwa uzushi mkubwa: {Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa} [4:156],

Wakamtuhumu Al-Twahira kwa uzinifu, Allah akamkosha na tuhuma ile, na akamuelezea Maryam kuwa: {Na mama yake ni mwanamke mkweli.} [5:75];

Muumini wa Unabii na ujumbe wa Issa (‘Alahyi Salaam).




Allah akamneemesha Mtume wake na mja wake Issa ('Alayhi salaam) na mama yake: {Na pale Mwenyezi Mungu atapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipo kutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani. Na nilivyo kufunza kuandika na hikima na Taurati na Injili…} [5:110],

Na akamtia nguvu kwa miujiza na alama: {…Na ulipo tengeneza udongo sura ya ndege, kwa idhini yangu, kisha ukapuliza ikawa ndege kwa idhini yangu; na ulipo waponesha vipofu na wakoma kwa idhini yangu; na ulipo wafufua wafu kwa idhini yangu; na nilipo kukinga na Wana wa Israili ulipo wajia na hoja zilizo wazi, na wakasema walio kufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu! Na nilipo wafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.} [5:110-111],

Kisha ni kuwa Al-Hawariyyuun (wafuasi wake) walimtaka Issa ('Alayhi salaam) amuombe Mola wake awateremshie chano cha kula kutoka mbinguni, Allah kasema: {Wanafunzi walipo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Je, Mola wako Mlezi anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni?...} [5:112],

Issa akawaogopea kutoshukuru kwao: {…Akasema: Mcheni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini. Wakasema: Tunataka kukila chakula hicho, na nyoyo zetu zitue, na tujue kwamba umetuambia kweli, na tuwe miongoni mwa wanao shuhudia.} [5:112-113],

Kwa hiyo akamuomba Mola wake: {Akasema Isa bin Maryamu: Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu! Tuteremshia chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe ni Ishara itokayo kwako. Basi turuzuku, kwani Wewe ndiye mbora wa wanao ruzuku. Mwenyezi Mungu akasema: Hakika Mimi nitakuteremshieni hicho. Lakini yeyote katika nyinyi atakaye kanya baadae, basi hakika Mimi nitampa adhabu nisiyopata kumpa yeyote katika walimwengu.} [5:114-115],



Hata hivyo baadhi ya walioteremshiwa walikufuru.

Ama Mayahudi katika Bani Israil waliomkadhibisha Nabii wa Allah Issa ('Alayhi salaam) kule kukufuru kwao na kukadhibisha kwao na vitimbi vyao viliendelea kwa Isa ('Alahyi Salaam): {Na Makafiri walipanga mipango na Mwenyezi Mungu akapanga mipango, na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa wenye kupanga.} [3:54],


Allah akamjulisha kuhusu vitimbi vyao, na jinsi ambavyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) atamuokoa kutokana nao:

{Pale Mwenyezi Mungu alipo sema: Ewe Isa! Mimi nitakufisha, na nitakunyanyua kwangu, na nitakutakasa na wale walio kufuru, na nitawaweka wale walio kufuata juu ya wale walio kufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nikuhukumuni katika yale mliyo kuwa mkikhitalifiana.} [3:55],

Na walipoendelea kuvunja ahadi, vitimbi, ukafiri wao, na jaribio lao la kuuwa manabii wa Allah na kumtuhumu Al-Twahira Maryam ('Alayha salaam) kwa uzushi Allah alisema: {Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi zao, na kuzikataa kwao ishara za Mwenyezi Mungu, na kuwauwa kwao Manabii bila ya haki, na kusema kwao: Nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru zao, basi hawaamini ila kidogo tu - Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa, Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu…} [4:155-157]

**Issa anasisitiza katika Injili kuwa Mungu ni mmoja.**

"Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza, Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? Yesu akamjibu, Ya kwanza ndio hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote." (Marko Mtakatifu 12:28-35). Huu ni usia wa kwanza.



Lakini Allah alimuokoa dhidi yao: {…nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu ….} [4:157]

Bali walimuua aliyefanana nae: {…bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini. Bali Mwenyezi Mungu alim- tukuza kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:157-158],

Allah akamuokoa Mtume wake Issa (‘Alayhi salaam) na kumnyanyua kwake:

{Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.} [4:159].





## Issa katika Uislamu

"Nilipousoma Uislamu nilipata sura nyingine tofauti za Masihi ('Alayhi Salaam) ambazo ziliingiza katika nafsi yangu athari kubwa."

**Frederick Dolamark.**

Mkuu wa Maaskofu Johannesburg.

Huu ndio ukweli wa kisa cha Issa ('Alayhi salaam):

{Huyo ndiye Isa mwana wa Maryamu. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka. Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwa na mwana, Subhanahu, Yeye ametakasika! Anapo lihukumia jambo basi huliambia tu: Kuwa! Likawa. } [19:34-35],

Kwa hiyo Allah kabainisha kuwa haifai Yeye kuwa na mtoto; kwa kuwa Yeye ni Muumba wa kila kitu na mmliki wake, na kila kitu kinahitaji na dhalili kwake, na wote mbinguni na ardhini ni waja wake, Yeye ndie Mola wao La ilaha illa Llah; ni Yeye na hakuna Mola mwingine asiyekuwa Yeye.

## Injili inakanusha kusulubiwa na inathibitisha Kuinuliwa Mbinguni.

"Basi wakaokota mawe ili wamtupie; lakini Yesu akajificha, akatoka hekaluni." (Yohana 8:59).
"Wakatafuta tena kumkamata; lakini akatoka mikononi mwao." (Yohana 10:39).
"Hili limetokea ili yatimie yaliyokuja kwenye kitabu: Hakuvunja chochote katika mfupa." (Yohana 36:19).
"Huyu Yesu huyu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni." (Matendo ya Mitume 1:11)



https://www.path-2-happiness.com/sw



## 5. MUHAMMAD (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni mwisho wa mitume na manabii, Issa – ('Alayhi salaam) amewabashiria Bani Israil kuja mtume wa mwisho, Allah amesema: {Na Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninaye thibitisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhaahiri!} [61:6],

Hivyo basi bishara ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ipo katika Taurati na Injili. Allah amesema: {Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.} [7:157],

Bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) amechukua ahadi na mkataba kwa manabii wamuamini Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) na wamnusuru yeye kama atatumwa kwao wakiwa hai, na wawaambie kaumu zao hilo ili habari yenyewe ienee baina ya Ummah zote, Allah

https://www.path-2-happiness.com/sw



amesema: {Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.} [3:81]

Qur-aan imeashiria bishara hizo, na kuthibitisha ukweli wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), Allah amesema: {Na walio kufuru wanasema: Wewe hukutumwa. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi, na pia yule mwenye ilimu ya Kitabu} [13:43],

Na katika aya nyingine: {Na hakika bila ya shaka haya yamo katika Vitabu vya kale. Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili? } [26:196-197]

Na akazungumzia kuhusu msimamo wa Ahlul kitab ambao ilipasa kuwa ndio



wa mwanzo na waumini kwa kumjua kwao kama walivyokuwa wakiwajua watoto wao: {Wale tulio wapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyo wajua watoto wao; na kuna kikundi katika wao huificha haki na hali wanajua.} [2:146],

Allah Mtukuka amesema: {Na alipo wajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kuthibitisha yale waliyo nayo, kundi moja miongoni mwa wale walio pewa Kitabu lilitupa Kitabu cha Mwenyezi Mungu hicho nyuma ya migongo yao kama kwamba hawajui.} [2:101],

Tabiri zile zikathibitika kwa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam), na kuwa yeye ndie Mtume ambae Allah amezungumzia kuja kwake, hata hivyo kundi moja miongoni mwao likaficha haki likiwa linajua, na wakiacha yaliyokuja kwenye vitabu vyao vitakatifu nyuma ya migongo yao kama kwamba hawafahamu.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuja na Tawhidi: Yaani kumpwekesha Allah peke yake bila kumshirikisha kama walivyo kuja Mitume na Manabii waliotangulia, Allah Mtukuka

amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.} [21:25],


Kama alivyotumwa kusadikisha Mitume na manabii waliotangulia, bila ya kutofautisha chochote katika kuwaamini wao: {…hatutafautishi baina ya yeyote katika hao…} [2:136],

Bali yule ambae atamsadiki na kumuamini Muhammad bila ya kuamini mtume yoyote au nabii aliokuja ndani ya Qur-aan-basi mtu hakumkubali wala kumuamini Muhammad: {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo.} [42:13]

Na akatia mkazo kuwa yeye ni mja wa Allah: {Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi.} [18:110],

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuwa ni Umiyyi hasomi wala haandiki (yaliyoandikwa) kama ilivyokuja sifa yake katika vitabu vilivyotangulia ili Ahlul Kitab wamtambue ambao wanajua sifa zake zilizokuja ndani ya vitabu vyao; kama alivyosema Allah (Subhaanahu






**Muhammad ...Mtume wa Mwisho.**

"Kwa sababu Mungu atanipandisha kutoka ardhini na atabadilisha mandhari ya haini hadi kila mmoja wenu atadhania: pamoja na hayo pindi anapokufa mtu muovu mimi nitakuwa katika fedheha muda mrefu Ulimwenguni, lakini kutokana na mimi atakapokuja Muhammad Mtume Mtukufu doa hili litaniondoka."

**Injili ya Barnaba.**



wa Ta'ala): {Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.} [7:157].

Allah alipitisha miujiza ile kwenye mikono yake kama alivyopitisha katika mikono ya Mitume kabla yake – miujiza mingi ilikuwa ni ya kuonekana japokuwa muujiza mkubwa zaidi ulikuwa ni Qur-aan tukufu ambayo na ni yake kuna habari za wa mwanzo na za wa mwisho, ubainifu, uongofu, rehma na bishara: {…Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.} [16:89],

Na uoni kwa waumini: {Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu wote, na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanao yakinisha.} [45:20],

Mtume Ummiy (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akawabainishia watu walichotofautiana ndani ya Qur-aan: {Na hatukukuteremshia Kitabu isipo kuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalifiana, na kiwe Uwongofu na Rehema kwa watu wanao amini.} [16:64].


Pamoja na makafiri wa kikureishi kujua ukweli wake na amana yake na kwa sababu tokea mwanzo walimuita 'Mkweli mwaminifu' lakini pamoja na hayo walimkadhibisha, Allah akawapa changamoto wakusanyike wote, watu kwa majini na walete mfano wa Qur-aan hii: {Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur-aani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.} [17:88],

Wakashindwa pamoja na uwezo wao wa lugha na akawapa changamoto nyingine baada ya kukusanyika walete aya kumi tu mfano wake: {Au wanasema: Ameizua? Sema: Basi leteni Sura kumi zilizo zuliwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli.} [11:13],

Wakashindwa na akawapa changamoto nyingine ya kuleta sura moja inayokaribiana nayo. {Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake…} [2:23];

Walishindwa pamoja na uwezo wao wa lugha.

Makafiri wa Kikureishi wakaendelea kumkadhibisha; Allah akamuamrisha kusubiri kama walivyosubiri Ulul 'Azm




**Injili inayotoa biashara ya Muhammad.**

"Itabakia hivi hadi atakapokuja Muhammad Mtume wa Mungu ambaye muda atakapofika atauweka wazi uongo kwa walioamini sheria ya Mungu. Na imekuja katika Isaya: Mimi nimefanya jina lako Muhammad Ewe Muhammad Ewe uliye mtakatifu kutoka kwa Mungu Jina lako lipo milele. Na katika Habakkuki imekuja (3:3-6): "Mungu alikuja kutoka Temami, yeye aliye mtakatifu kutoka mlima Parani. Utukufu wake ukaangaza mbingu kutokana na haiba ya Muhammad, nayo dunia ikajaa sifa yake. Au kama ilivyokuja katika Isaya: Nilichompa sitompa mwingine. Ahmad (jina lingine la Muhammad) anamhimidi Mungu mazungumzo yenye kuja kutoka kwa watu bora duniani: Viumbe watafurahi kwayo na kumtakasa kila kitukufu na kuadhimisha kila sehemu."

**injili ya Barnaba**


katika mitume na manabii kabla yake: Ibrahim, Nuuh, Musa na Issa ('Alayhi salaam) wote: {Basi subiri, kama walivyo subiri Mitume wenye stahmala kubwa…} [46:35]

Akasubiri na akaendelea na da'wah yake akiwalingania na kuwafundisha maneno yake na maneno ya Muumba wake, Allah akamtosheleza na kumlinda: {Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na Waumini walio kufuata.} (8:64), {Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtosheleza mja wake?...} [39:36]

Allah akamnusuru kama alivyowanusuru Mitume wengine: {Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.} [58:21],

Akasema Mtukuka: {Na bila ya shaka neno letu lilikwisha tangulia kwa waja wetu walio tumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakao nusuriwa. Na kwamba jeshi letu ndilo litakalo shinda. } [37:171-173], {Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi} [40:51].

Makafiri wakataka kuzuia ujumbe wake na kuzima nuru yake, lakini Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) akatimiza



## Kiigizo Chema na mfano wa juu.

"Nimetafuta katika historia mfano wa juu wa mtu huyu. Nikaupata kwa Nabii Muarabu Muhammad."

Mwandishi na mshairi wa Ujerumani.

**Goethe**




## Uliza na Qur-aan itakujibu.

"Nimesoma Qur-aan nikapata majibu kwa kila swali linalohusu maisha."

**Michael Hart.**

Mwandishi wa Kimarekani.



**Na kwa watu ni Ahmad.**

"Hakika ule msemo maarufu wa Kikristo: Utukufu ni kwa Mungu aliye juu. Katika ardhi ni amani, na kwa watu ni furaha. Haikuwa hivi, bali ilikuwa: Utukufu ni kwa Mungu aliye juu na katika ardhi ni amani na kwa watu ni Ahmad."

**David Benjamin Kelden**

Kiongozi Mkuu wa Wakristo
Mosol-Iraq

neema yake: {Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapo kuwa makafiri watachukia. Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya haki ili ipate kuzishinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia. } [61:8-9].

Akakamilisha neema yake na kuudhihirisha Uislamu, akatilia mkazo juu ya Tawhidi ya Allah katika dini zote, akakamilisha neema yake kwa wanadamu kwa ujumbe huu na dini hii: {…Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini…} [5:3],

Bali aliihifadhi dini hii, na akaufanya ujumbe huu kubakia hadi Siku ya Kiama: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9];

Kwa hiyo huu ni ujumbe hitimisho wa ujumbe wote: {Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu} [33:40],

Nao ni ujumbe wenye kubakia hadi pale ambapo Allah atairithi ardhi hii na waliomo.

Basi ni ujumbe gani huu wenye kubakia kwa hifadhi ya Allah hadi Siku ya Malipo…..?!

## Qur-aan ni muujiza.

"Qur-aan inaongoza fikra na kukamata nyoyo, imeshuka kwa Muhammad dalili ya ukweli wake."

**Henri de Castriesry.**
Luteni wa zamani wa jeshi la Kifaransa.

